**SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR**

# HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA
# MHESHIMIWA NASSOR AHMED MAZRUI (MBM)

# KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

***Juni, 2023***

## YALIYOMO

*Mada* *Ukurasa*


MAELEZO YA VIFUPISHO .................................................................. iii

UTANGULIZI ........................................................................................ 1

UTEKELEZAJI WA KIFEDHA KWA MWAKA 2022/2023 ......................... 2

MAFANIKIO YA WIZARA KWA MWAKA FEDHA 2022/2023 ......... 5

PROGRAMU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA (PH0101) .......................... 6

HUDUMA SHIRIKISHI ZA UKIMWI, HOMA YA INI, KIFUA KIKUU NA UKOMA 8

HUDUMA ZA KUMALIZA MALARIA ZANZIBAR ........................................... 12

HUDUMA SHIRIKISHI ZA AFYA YA UZAZI YA MAMA NA MTOTO ................. 13

HUDUMA ZA MARADHI YASIYOAMBUKIZA ................................................ 16

HUDUMA YA UFUATILIAJI WA MIENENDO YA MARADHI ........................... 18

HUDUMA ZA MARADHI YASIYOPEWA KIPAUMBELE .................................. 19

HUDUMA ZA MSINGI ZA MATIBABU YA MACHO ....................................... 20

HUDUMA YA UTOAJI WA ELIMU YA AFYA ................................................. 21

HUDUMA ZA AFYA YA MAZINGIRA ........................................................... 22

HUDUMA ZA AFYA BANDARINI ................................................................. 23

HUDUMA YA AFYA YA WAFANYAKAZI ....................................................... 24

HUDUMA ZA AFYA YA MSINGI YA AKILI ..................................................... 25

HUDUMA ZA BARAZA LA WATAALAMU WA AFYA YA JAMII
NA MAZINGIRA ............................................................................................ 25

PROGRAMU YA HUDUMA ZA TIBA (PH0102) ............................ 26

PROGRAMU NDOGO YA HUDUMA ZA MATIBABU ........................... 28

HUDUMA ZA USHIRIKIANO WA AFYA KIMATAIFA ..................................... 29

HUDUMA ZA DAMU SALAMA ........................................................ 30

HUDUMA ZA MKONO KWA MKONO (ONE STOP CENTRE) ........................ 30

HUDUMA ZA BODI NA MABARAZA YA KITAALUMA ......................... 31

HUDUMA ZA USHAURI HOSPITAL BINAFSI ............................................... 31

HUDUMA ZA BARAZA LA WATAALAMU WA MAABARA ZA TIBA ................ 31

HUDUMA YA TIBA ASILI NA TIBA MBADALA .............................................. 32

HUDUMA ZA MADAKTARI ......................................................................... 33

HUDUMA ZA WAUGUZI NA WAKUNGA .................................................... 33

HUDUMA ZA UPATIKANAJI, UHIFADHI, USAMBAZAJI WA
DAWA ZA VIFAA TIBA ................................................................................. 34

OFISI ZA MFAMASIA MKUU WA SERIKALI ........................................................ 34
IDARA ZA BOHARI KUU YA MADAWA ................................................................ 35
PROGRAMU NDOGO HUDUMA ZA UCHUNGUZI (SH030202) ..................... 37
HUDUMA ZA WAKALA WA CHAKULA NA DAWA ........................................ 37
HUDUMA ZA WAKALA WA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI .... 38
PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA (PH0103) ...... 39
PROGRAMU NDOGO YA UTAWALA NA UENDESHAJI (SH010301) ........ 39
NGUVU KAZI YA SEKTA YA AFYA ....................................................................... 39
HUDUMA YA AFYA KIDIJITALI .......................................................................... 40
USIMAMIZI WA SHERIA ...................................................................................... 42
PROGRAMU NDOGO YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI (SH010302) ..... 43
TAASISI YA UTAFITI WA AFYA (ZAHRI) ................................................. 47
PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA WIZARA YA
AFYA PEMBA (SH010303) ....................................................................... 47
PROGRAMU YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA (HO2) ......................... 49
PRGOGRAMU NDOGO YA UCHUNGUZI NA MATIBABU (SH020101) .... 50
PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA HOSPITALI
YA MNAZI MMOJA (PH0202) ................................................................. 52
UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ........................................ 53
CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 54
MWELEKEO WA BAJETI NA VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA
MWAKA 2023/2024 .................................................................................. 55
SHUGHULI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA NA WIZARA YA
AFYA KWA MWAKA 2023/2024 ............................................................. 55
MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 ............. 56
PROGRAMU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA (PH0101) ......................... 56
PROGRAMU YA TIBA (PH0102) ............................................................. 58
PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA AFYA
(PH0103) ................................................................................................ 59
PROGRAMU YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA (H02) ......................... 60
SHUKRANI ............................................................................................. 61
HITIMISHO ............................................................................................. 62
MAOMBI YA FEDHA KWA UTEKELEZAJI WA KAZI ZILIZOPANGWA
KWA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 ... 63

## MAELEZO YA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| ARV | - | Anti-Retroviral Virus |
| BADEA | - | Arab Bank for Economic Development in Africa |
| BOQ | - | Bill of Quantities |
| CBM | - | Christian Blind Mission |
| CCM | - | Chama cha Mapinduzi |
| CDC | - | Centre for Disease Control and Prevention |
| CHVs | - | Community Health Volunteers |
| CTCs | - | Care and Treatment Clinics |
| Danida | - | Danish International Development Agency |
| DFID | - | Department for International Development |
| DHIS2 | - | District Health Information System |
| DNA | - | Deoxyribonucleic Acid |
| EAC | - | East African Community |
| e-IDSR | - | electronic Integrated Disease Surveillance and Response |
| e-LMIS | - | electronic Logistic Management Information System |
| EMR | - | Electronic Medical Records |
| ENT | | Ear Nose and Throat |
| GFATM | - | Global Fund to Fight AIDS, Tuberculosis and Malaria |
| HIPZ | - | Health Improvement Project Zanzibar |
| IMF | - | International Monitory Fund |
| JICA | - | Japan International Cooperation Agency |
| JKCI | - | Jakaya Kikwete Cardiac Institute |
| JKU | - | Jeshi la Kujenga Uchumi |
| KMKM | - | Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo |
| AMREF | - | Africa Medical Research Foundation |
| MOI | - | Muhimbili Orthopedic Institute |
| MUHAS | - | Muhimbili University of Health and Allied Sciences |
| PEPFAR | - | President’s Emergency Plan for AIDS Relief |

| | | |
|---|---|---|
| PHL | - | Public Health Laboratory |
| PMI | - | President's Malaria Initiatives |
| RCH | - | Reproductive and Child Health |
| SMZ | - | Serikali ya Mapinduzi Zanzibar |
| SOP | - | Standard Operating Procedures |
| SRS | - | Software Requirements Specification |
| STBF | - | Susan Thompson Buffet Foundation |
| TEHAMA | - | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| THPS | - | Tanzania Health Promotion Support |
| TV | - | Television |
| UAE | - | United Arab Emirates |
| UK | - | United Kingdom |
| UKIMWI | - | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| UNDP | - | United Nations Development Program |
| UNFPA | - | United Nations Population Fund |
| UNICEF | - | United Nations International Children Emergency Fund |
| USAID | - | United States Agency for International Development |
| UTI | - | Urinary Track Infection |
| VVU | - | Virusi Vya UKIMWI |
| WHO | - | World Health Organization |
| ZAHRI | - | Zanzibar Health Research Institute |
| ZanEMR | - | Zanzibar Electronic Medical Record |
| ZBC TV | - | Zanzibar Broadcasting Cooperation Television |
| ZBS | - | Zanzibar Bureau of Standards |
| ZCTV | - | Zanzibar Cable Television |
| ZFDA | - | Zanzibar Food and Drug Agency |
| ZOP | - | Zanzibar Outreach Programme |

## UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Kwanza kabisa naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma aliyeumba mbingu na ardhi na vyote vilivyomo baina yake, kwa kutujaalia uhai, uzima na afya njema; hali iliyopelekea kukutana tena katika kikao hiki kujadili bajeti ya Wizara ya Afya.

2. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, natoa shukrani za pekee kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi **Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi** kwa kuendelea kuliongoza vyema Taifa hili katika hali ya amani na utulivu. Pia, niwapongeze **Mheshimiwa Othman Masoud Othman** Makamo wa Kwanza wa Rais na **Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah** Makamo wa Pili wa Rais kwa mashirikiano mazuri wanayompatia katika kuiongoza nchi yetu.

3. **Mheshimiwa Spika,** Nichukuwe fursa hii kukupongeza wewe binafsi, kwa kuendelea kuliongoza Baraza hili kwa umakini kabisa. Pia nawapongeza Naibu Spika, Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma na Wenyeviti wa Baraza hili Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma na Mheshimiwa Abdalla Hussein Kombo kwa kukusaidia katika kuendesha mijadala mbali mbali ndani ya Baraza hili, kazi ambayo wameifanya kwa umahiri mkubwa. Aidha, nampongeza Katibu wa Baraza la Wawakilishi, Ndugu Raya Issa Msellem kwa kusimamia na kufanikisha shughuli za Baraza kwa ufanisi.

4. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa Wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii inayoongozwa na Mheshimiwa Mohammed Ahmada (Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Malindi), hivyo nachukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa namna walivyoshirikiana nasi wakati wote walipofanya ziara katika Wizara hii, wameonesha uweledi na ukomavu mkubwa katika kutupatia maelekezo, ushauri na mapendekezo ya kuimarisha utendaji kazi kwa nia ile ile ya kufikia malengo ya Serikali ya Awamu ya nane (8). Baada ya shukurani hizo sasa kwa ruhusa yako naomba nieleze utekelezaji wa Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kama ifuatavyo: -

**UTEKELEZAJI WA KIFEDHA KWA MWAKA 2022/2023**

5. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Afya, (Fungu H01) ilikadiriwa kutumia shilingi **154,027,109,000/=** zikijumuisha shilingi **35,109,700,000/=** kwa ajili ya mishahara; shilingi **53,493,100,000/=** kwa kazi nyenginezo; shillingi **4,698,800,000/=** kwa Ruzuku na shilingi **60,725,509,000/=** kwa kazi za Maendeleo. Aidha, Hospitali ya Mnazi Mmoja (Fungu H02) ilikadiriwa kutumia shilingi **34,186,349,000/=** zikihusisha shilingi **14,694,200,000/=** kwa ajili ya mishahara na shilingi **5,969,930,000/=** kwa kazi za uendeshaji wa Hospitali na shilingi **13,522,219,000/=** kwa Miradi ya maendeleo.

6. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2023, Wizara ya Afya (Fungu H01) iliingiziwa na kutumia jumla ya shilingi **71,340,303,535/=** sawa na asilimia **46.3** ya makadirio kwa mwaka

2022/2023. Kati ya hizo shilingi **40,523,419,920/=** kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia **115,** Ongezeko hili ni kutokana na mabadiliko ya mishahara yalioanza Julai 2022, shilingi **17,315,367,591/=** kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na asilimia **32.3** na shilingi **3,510,461,425/=** kwa ajili ya ruzuku sawa na asilimia **74.7**. Aidha, shilingi **9,991,054,599/=** sawa na asilimia **16.4**, ziliingizwa na kutumika kwa kazi za maendeleo, kati ya hizo shilingi **1,893,738,719/=** sawa na asilimia **7.5**, kutoka Serikalini, na shilingi **8,097,315,880/=** sawa na asilimia **32.1**, kutoka kwa washirika wa maendeleo. Mchanganuo wa fedha hizo unapatikana katika **kiambatisho namba 1.**

7. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa hospitali ya Mnazi Mmoja (H02) shilingi **19,507,633,243/=** zilipatikana na kutumika. Fedha hizo zinajumuisha shilingi **2,138,619,900/=** kwa matumizi ya mengineyo sawa na asilimia **44.3** na shilingi **17,369,013,343/=** sawa na asilimia **118** kwa ajili ya mishahara. Ongezeko hili ni kutokana na mabadiliko ya mishahara yalioanza Julai 2022**. Kiambatisho namba 1** kinatoa ufafanuzi.

8. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Afya (Fungu H01) ilikadiriwa kukusanya shilingi **25,000,000,000/=,** Hadi kufikia Machi 2023 makusanyo ya Wizara ya Afya yamefikia shilingi **2,301,627,251/=** sawa na asilimia **9.2** ya makadirio. Makusanyo yameshuka kutokana na kupungua kwa maambukizi ya UVIKO 19. **Kiambatisho namba 2**.

9. **Mheshimiwa Spika,** Hospitali ya Mnazi Mmoja (Fungu H02) kwa 2022/2023 ilikadiriwa kukusanya shilingi **1,000,000,000/=** kupitia vyanzo vya malipo ya huduma za Afya, huduma za haraka (Fast Track) huduma za Bima na malipo ya wanafunzi wa kigeni. Hadi kufikia Machi, 2023 Hospitali ya Mnazi Mmoja imekusanya jumla ya shilingi **707,106,743/=** sawa na asilimia **70.7**, makusanyo hayo yanaonekana kwenye **kiambatisho namba 2.**

10. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kupata fedha za ahueni ya UVIKO 19 ambazo ni shilingi **37,315,563,560/=** ambazo zilitumika kutoka fedha zilizoidhinishwa. Aidha, Hospitali ya Mnazi Mmoja imeingiziwa fedha maalumu shilingi **2,130,000,000/=** kwa matumizi ya dawa na vifaa tiba na shilingi **597,405,350/=** ziliingizwa kwa matumizi ya tiba hewa (gesi ya oksijeni), ambazo ni fedha kutoka Wizara ya Afya.

11. **Mheshimiwa Spika,** Vipaumbele vya Wizara vimezingatia mapendekezo yaliyotolewa katika mapitio ya utekelezaji ya Wizara kwa mwaka 2022/2023, Mpango Mkakati wa nne wa Wizara, Mikakati ya Kitaifa na Kimataifa, Dira ya Maendeleo 2050, Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020/2025 na maagizo ya Serikali. Vipaumbele hivyo vinagusa maeneo yafuatayo: -

    i. Kuimarisha Huduma na miundombinu ya Afya ya Uzazi ya Mama na mtoto kwa kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto wachanga,

    ii. Kuimarisha upatikanaji wa Dawa, vifaa tiba na uchunguzi,

iii. Kuanzisha kwa mfuko wa huduma za afya Zanzibar,

iv. Kuimarisha nguvu kazi ya Afya,

v. Kuimarishwa huduma za Afya ya Msingi,

vi. Kuimarisha kinga na kuendeleza mapambano dhidi ya maradhi ya mripuko na majanga ya kiafya,

vii. Kuendeleza mapambano dhidi ya maradhi ya kuambukiza na yasiyoambukiza,

viii. Kuimarisha miundombinu ya utoaji wa huduma za afya,

ix. Kuimarisha matumizi ya taarifa za afya katika kufanya maamuzi.

## MAFANIKIO YA WIZARA KWA MWAKA FEDHA 2022/2023

12. **Mheshimiwa Spika,** yafuatayo ni baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 kama ifuatavyo: -

i. Kuimarisha Afya ya Uzazi wa Mama na mtoto na kupunguza vifo vya mama wajawazito kutoka mama **70** kwa 2021 hadi **56** kwa mwaka 2022. Vilevile, Jumla ya vichanga vilivyofariki **1,973** viliripotiwa kwa mwaka 2021, ikilinganishwa na vichanga **1,716** vilivyofariki mwaka 2022,

ii. Kuongeza upatikanaji wa Dawa, vifaa tiba na uchunguzi,

iii. Kuanzishwa kwa Mfuko wa Huduma za Afya kwa wote,

iv. Kuimarisha nguvu kazi ya Afya kwa kuajiri jumla ya wafanyakazi wapya 710 kwa mwaka 2022/2023,

v. Kuimarisha huduma za Afya ya Msingi,

vi. Kuimarisha kinga na kuendeleza mapambano dhidi ya maradhi ya mripuko na majanga ya kiafya,

vii. Kuendeleza mapambano dhidi ya maradhi ya kuambukiza na yasiyoambukiza,

viii. Kuimarisha miundombinu ya utoaji wa huduma za afya ikiwemo kukamilika kwa ujenzi wa hospital 10 za Wilaya na Hospital moja (1) ya Mkoa pamoja na jengo la Maabara ya Wakala wa Chakula, Dawa,

ix. Kuendelea kukusanya na kuzitumia taarifa za afya na kufanya maamuzi sahihi kwa kutumia miongozo mbalimbali ya utekelezaji.

13. **Mheshimiwa Spika,** Mafanikio haya na mengineyo yanaelezwa kwa kina katika utekelezaji wa shughuli zilizofanyika kupitia huduma zinazotolewa katika kila programu husika kama ifuatavyo:-

**PROGRAMU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA (PH0101)**

14. **Mheshimiwa Spika,** jukumu la Programu hii ni kuhakikisha jamii inapata huduma bora za kinga pamoja na kuongeza uelewa kwa njia mbalimbali za kujikinga na maradhi ya kuambukiza na yasioambukiza. Katika kufikia azma hii Wizara kupitia Programu ya Kinga na Elimu ya Afya ilipanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuimarisha huduma za afya ya mama na mtoto ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi pamoja na vifo vya watoto wachanga.

ii. Kuendelea kudhibiti maambukizi ya virusi vya UKIMWI, homa ini na kifua kikuu.

iii. Kuendelea na mikakati ya kumaliza Malaria hasa katika maeneo ambayo bado maambukizi ya maradhi hayo yanaripotiwa.

iv. Kuongeza kiwango cha chanjo kwa watoto waliochini ya mwaka mmoja kufikia zaidi ya asilimia **90**.

v. Kuendelea kutoa chanjo ya saratani ya shingo ya kizazi kwa watoto wa kike wenye umri wa miaka 9 hadi 14.

vi. Kuhamasisha jamii juu ya usafi wa mazingira ili kujikinga na maradhi mbali mbali yakiwemo maradhi ya kuharisha na kipindupindu.

vii. Kuendeleza Programu za elimu ya afya katika ngazi ya jamii na maskulini.

viii. Kufuatilia mienendo ya maradhi ili kuweza kubaini mapema uwepo wa maradhi na kuchukua tahadhari zinazostahiki

ix. Kuimarisha huduma za kinga dhidi ya maradhi ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza.

x. Kutekeleza mkakati wa kimataifa wa kudhibiti maradhi (International Health Regulation –IHR)

**15. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Afya kupitia fungu **(PH0101)** ilitenga jumla ya shilingi **34,410,113,000/=** Kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa kupitia Programu ya Kinga na Elimu ya Afya ambapo hadi kufikia Machi 2023 kiasi cha shilingi **15,768,477,573/=** zilitumika sawa na asilimia **45.8** ya fedha

zilizotengwa katika programu hii. Utekelezaji wa shughuli zilizoainishwa katika programu hii unaelezwa kupitia huduma mbali mbali zilizotolewa kama ifuatavyo: -

**HUDUMA SHIRIKISHI ZA UKIMWI, HOMA YA INI, KIFUA KIKUU NA UKOMA**

**16. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ilitenga jumla ya shilingi **5,038,603,000/=,** kati ya hizo shilingi **94,288,000/=** ni kutoka Serikalini na shilingi **4,645,200,000/=** kutoka kwa washirika wa maendeleo. Hadi kufikia Machi 2023, huduma hii imepokea kiasi cha shilingi **2,052,334,569/=** kutoka kwa washirika wa maendeleo sawa na asilimia **44.1**.

**17. Mheshimiwa Spika,** Kuanzia Julai 2022 hadi Machi, 2023. Jumla ya watu **93,912** (wanawake **50,310** na wanaume **43,602**) walipatiwa huduma za ushauri nasaha na upimaji wa VVU katika vituo mbali mbali vya afya vya Unguja na Pemba, kati ya hao **659** (Wanawake **416** na wanaume **243**) sawa na asilimia **0.7** wamebainika kuwa na maambukizi ya VVU. Aidha, watu wa makundi maalumu **7,313** walipatiwa huduma ya upimaji wa VVU na jumla ya watu **174** sawa na asilimia **2.4** waligundulika kuwa na maambukizi ya VVU na kuanzishwa huduma za kupunguza makali ya VVU (ARVs).

**18. Mheshimiwa Spika,** Katika kudhibiti maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, jumla ya mama **43,357** walihudhuria kliniki kwa mara ya kwanza na kupatiwa huduma ya

upimaji wa VVU, ambapo mama **41,638** sawa na asilimia **96** walipatiwa huduma ya upimaji wa VVU kati ya hao mama **264** sawa na asilimia **0.6** waligundulika na maambukizo ya VVU, mama wote wajawazito waliobanika na maambukizi walipewa dawa za kupunguza makali ya VVU (ARVs). Aidha, watoto **212** waliozaliwa na mama wenye maambukizi ya VVU walipimwa VVU kwa kutumia machine ya DNA-PCR ambapo jumla ya watoto 3 sawa na asilimia **1.4** walibainika kuwa na maambukizi ya VVU.

**19.** **Mheshimiwa Spika,** hadi sasa jumla ya wateja **8,417** (wanaume **2,603** na wanawake **5,815**) wanaoishi na VVU wanapatiwa huduma kwenye kliniki zetu za huduma na tiba kwa waathirika wa VVU (CTCs) Kupitia vituo vya afya **14** (Unguja **10** na Pemba **4**). Miongoni mwa watu hao; **8,263** (wanawake **5,720** na wanaume **2,543**) sawa na asilimia **98** ya wenye maambukizi na wanaotumia dawa za kupunguza makali ya VVU (ARVs) wanazopatiwa kutoka kwenye kliniki hizo za huduma na tiba (CTCs).

**20.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kutoa huduma bora kwa wananchi Wizara inafuata malengo ya Dunia ya “95, 95, 95” ifikapo mwaka 2030 hii inamaanisha asilimia **95** ya watu wanaoishi na maambukizi ya VVU **8,417/10,580** sawa na asilimia **79.6** wanajijua hali zao za maambukizi kati ya hao asilimia 95 ya watu **8,263/8,417** ni sawa na asilimia **98.2** wawe wanatumia dawa yakupunguza makali ya VVU na asilimia **95** ya hao wawe wamepungua au kupunguza makali ya VVU kiwango cha VVU **1,669/1,740** sawa na asilimia **95.9** hadi chini ya kopi 1,000.

21. **Mheshimiwa Spika,** Zoezi la ufuatiliaji wa wagonjwa wa VVU waliopo katika matibabu lilifanyika. Jumla ya sampuli za damu **2,692** zimekusanywa na kuangaliwa kiwango cha VVU katika Hospitali za Mnazi Mmoja, Kivunge na Chake Chake. Kati ya sampuli zilizochunguzwa, sampuli **1,669** sawa na asilimia **95.9** zimeonekana kuwa na kiwango cha chini ya kopi **1,000** na **1,504** chini ya kopi **50** na **71** juu ya kopi **1,000** ya kupunguza makali ya VVU kiwango cha virusi (Viral Load Supression).

22. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha utoaji wa huduma za kliniki ya "methadone", jumla ya wateja **1,596** (Wanaume **1,516** na wanawake **80**) wamesajiliwa. Hadi sasa jumla ya wateja **860** (wanaume **821** na wanawake **39**) wanaendelea na matibabu katika kliniki hiyo iliyopo Hospitali ya Wagonjwa wa Akili Kidongo Chekundu. Aidha, idadi ya wateja wapya wanaopata matibabu ya kuacha kutumia madawa ya kulevya "Methadone" imeongezeka kutoka **86** kwa mwaka 2021/2022 na kufikia watu **136** (wanaume **131** na wanawake **5**) kwa mwaka 2022/2023, ambapo jumla ya wateja **37** (Wanaume **33** na Wanawake **4**) walipona na kuruhusiwa.

23. **Mheshimiwa Spika,** hadi sasa jumla ya wagonjwa 1,654 wamesajiliwa na wanaendelea na matibabu ya homa ya Ini B katika kliniki za Mnazi Mmoja, Hospitali ya Kivunge na Hospitali ya Chake Chake. Jumla ya wagonjwa **87** (**70** wanaume na **17** wanawake) wenye maambukizo ya homa ya Ini 'B' wanaendelea na matibabu ya kupunguza makali virusi vya homa ya ini B. Vilevile, kwa upande

wa Homa ya Ini C, jumla ya wagonjwa wapya **81** (**67** wanaume na **14** wanawake) wamebainika kuwa na maambukizi ya Homa ya Ini C kwa Unguja na Pemba.

**24. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa maambukizi ya Kifua kikuu nayo yanaendelea kupungua ambapo jumla ya wagonjwa wapya **713** (Unguja **514** na Pemba **199**) wamegundulika kuwa na maambukizi ya Kifua Kikuu. Wagonjwa **612** sawa na asilimia **8** waligundulika na kifua cha ndani ya mapafu na wagonjwa **101** sawa na asilimia **14** waligundulika na kifua cha nje ya mapafu. Kati ya wagonjwa hao jumla ya wagonjwa **5** wamegundulika kuwa na Kifua Kikuu sugu. Wagonjwa wote wamepatiwa matibabu, kati ya wagonjwa wote wa Kifua kikuu hata hivyo, jumla ya wagonjwa **55** sawa na asilimia **8** ya wagonjwa waliochunguzwa wamegundulikana na maambukizi ya VVU na wote wameanzishiwa dawa za ARVs.

**25. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi hiki cha utekelezaji kutoka Julai 2022 hadi Machi 2023, Jumla ya wagonjwa wa Ukoma **78** (Unguja **69** na Pemba **9**) waligundulika, miongoni mwao wagonjwa **62** sawa na asilimia **69** waligundulika na Ukoma wenye mabaka mengi ambao unaambukiza katika jamii na wagonjwa **16** sawa na asilimia **21** ni wenye mabaka kidogo ambao hawaambukizi. Kati ya wagonjwa wote waliogundulika na Ukoma **62** sawa na asilimia **69** hawakuwa na ulemavu, **11** sawa na asilimia **14** walikuwa na ulemavu daraja la kwanza na **tano** sawa na asilimia **sita** walikuwa na ulemavu daraja la pili.

## HUDUMA ZA KUMALIZA MALARIA ZANZIBAR

26. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ilitenga jumla ya shilingi **3,935,774,000/=** kati ya hizo shilingi **513,352,000/=** ni kutoka Serikalini na shilingi **3,422,422,000/=** kutoka kwa washirika wa maendeleo. Hadi kufikia Machi 2023 huduma hii imepokea kiasi cha shilingi **2,503,451,626/=** kutoka kwa washirika wa maendeleo sawa na asilimia **73**.

27. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Afya inaendelea kuchukua hatua mbali mbali za kutokomeza Malaria Zanzibar, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, jumla ya watu **235,862** (Unguja 205,553 na Pemba 30,309) walichunguzwa vimelea vya malaria; Kati yao, Wagonjwa **2,194** (Unguja 1,192 na Pemba 202) sawa na asilimia **0.9** waligunduliwa kuwa na vimelea vya ugonjwa wa Malaria na walipatiwa matibabu stahiki. Hata hivyo wagonjwa **1,893** sawa na asilimia **86** ya waliobainika kuwa na vimelea vya Malaria walifuatiliwa majumbani kwa lengo la kuangalia chanzo cha maambukizo yao. Aidha, maeneo yaliyoripotiwa kuwa na wagonjwa wengi wenye vimelea vya Malaria ni kutoka Wilaya za Mjini, Magharibi B na Kati.

28. **Mheshimiwa Spika,** Takwimu za hapo juu zinaonyesha kushuka kwa maambukizi ya ugonjwa wa Malaria ambapo kwa mwaka 2021/2022, Jumla ya Watu **440,715** (Unguja 379,892 na Pemba 60,823) walichunguzwa vimelea vya malaria, ambapo wagonjwa **6,626** (Unguja 6,090 na Pemba 536) sawa na asilimia **1.5** waligunduliwa kuwa na vimelea vya ugonjwa wa Malaria.

29. **Mheshimiwa Spika,** Zoezi la upigaji Dawa Majumbani lilifanyika katika Shehia **49** za Unguja kwa Wilaya za Magharibi A, Magharibi B, Kati na Kusini. Zoezi hili limefanyika katika Wilaya hizo kutokana na kiwango kikubwa cha wagonjwa wa Malaria. Jumla ya nyumba **43,500** kati ya **45,000** zilizokadiriwa sawa na asilimia **97** zimepigwa dawa. Vilevile zoezi la kuua viluilui linaendelea kwa kutibu madimbwi na mabwawa yanayoonekana na viluilui vya mbu wa Malaria.

30. **Mheshimiwa Spika,** Katika hatua nyengine zoezi la ugawaji wa vyandarua linaendelea kwa Mama wajawazito na Watoto chini ya mwaka mmoja katika vituo vyote vya Serikali vinavyotoa huduma za Mama na Mtoto. Jumla ya vyandarua **73,342** viligaiwa. Kati ya hivyo vyandarua **38,631** viligaiwa kwa mama mjamzito kwenye hudhurio lake la mwanzo la ujauzito wake na vyandarua **34,711** viligawiwa kwa watoto waliopata chanjo ya Surua dozi ya mwanzo.

**HUDUMA SHIRIKISHI ZA AFYA YA UZAZI YA MAMA NA MTOTO**

31. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ilitenga jumla ya shilingi **3,233,566,000/=** kati ya hizo shilingi **1,517,588,000/=** ni kutoka Serikalini na shilingi **1,715,978,000/=** kutoka kwa washirika wa maendeleo. Hadi kufikia Machi 2023 huduma hii imepokea kiasi cha shilingi **2,193,919,091/=** kutoka kwa washirika wa maendeleo sawa na asilimia **67.8**

32. **Mheshimiwa Spika,** Katika jitihada za kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto wachanga Zanzibar, Wizara ya Afya inaendelea na hatua mbali mbali ikiwemo kufanya uhakiki wa vifo vya mama na mtoto kwa madhumuni ya kubainisha sababu zilizopelekea kutokea kwa vifo hivyo, kuhamasisha kina Mama kuhudhuria kliniki mapema na kujifungulia katika hospitali na vituo vya afya, pia kuwahamasisha akina Baba kuwasindikiza au kuwawahisha wake zao kliniki mapema na kuendelea kuhudhuria kliniki baada ya kujifungua. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, jumla ya vifo vya mama 46 na vifo vya watoto wachanga chini ya siku saba 1,567 viliripotiwa. Aidha, vifo vya mama 46 sawa na asilimia 100 na vifo vya watoto wachanga 840 sawa na asilimia 54 vilihakikiwa.

33. **Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya uhakiki huo yamebainisha sababu za vifo hivyo ni pamoja na watoto kukosa hewa wakati wa kuzaliwa; uzito pungufu; matatizo yatokanayo na mtoto njiti; kupoteza damu na maambukizi kwa watoto wachanga. Kwa upande wa vifo vya mama ni kifafa cha mimba, upungufu wa damu na kutokwa au kupoteza damu nyingi wakati wa ujauzito, kisukari pamoja na maradhi mengine sugu.

34. **Mheshimiwa Spika,** Katika kufanya juhudi za kuwashajihisha akina Mama kuhudhuria kliniki ya wajawazito pamoja na kujifungulia katika hospitali na vituo vya afya zimeendelea kuchukuliwa na kuonesha mafanikio. Jumla ya Mama na Wajawazito **52,891** walihudhuria kliniki ya upimaji mimba angalau mara moja katika

kipindi cha ujauzito, kati yao jumla ya Mama **9,017** walihudhuria kliniki wakiwa na ujauzito chini ya wiki 12 (sawa na asilimia 17). Aidha, katika kipindi hicho, Jumla ya Wajawazito **38,097** (Unguja 26,405 na Pemba 11,692) wote walijifungulia Hospitali.

35. **Mheshimiwa Spika,** Juhudi mbali mbali zinaendelea kuchukuliwa ili kupunguza vifo vitokanavyo na Mama na Mtoto, shirika la afya duniani limethibitisha kuwa matumizi ya njia za uzazi wa mpangilio yanaweza kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kwa zaidi ya asilimia 30. Kwa kipindi kuanzia mwezi wa July 2022 hadi machi 2023, jumla ya mama **23,644** wapya walijiunga na njia mbali mbali za kisasa za Uzazi wa mpangilio idadi hii imepungua ukilinganisha na mama **24,104** kwa kipindi kama hicho mwaka uliopita.

36. **Mheshimiwa Spika,** Kama nilivyoeleza mwanzoni mwa programu hii kwamba moja ya lengo la Wizara ni kuikinga jamii dhidi ya maradhi mbali mbali ambayo yanaweza kuepukika. Wizara imeendelea kutoa chanjo kwa watoto chini ya umri wa mwaka mmoja, ambapo watoto **45,016** walipatiwa chanjo ya Penta 3 na wasichana **18,529** wenye umri wa miaka 14 walipatiwa chanjo ya saratani ya mlango wa shingo ya kizazi. Aidha katika kuendelea na mapambano ya maradhi ya ulemavu wa ghafla kwa watoto chini ya umri wa miaka 5 jumla ya watoto **363,130** walipatiwa chanjo ya polio Unguja na Pemba kupitia zoezi maalumu la chanjo hiyo kama inavyojionesha kwenye **kiambatisho nambari 3a**. Sambamba na hilo, jumla ya watu **299,791** (Pemba **80,187** na Unguja **219,604**) walipatiwa chanjo ya UVIKO 19.

37. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha huduma za lishe Wizara imefanya zoezi maalumu ya ulishaji wa matone ya Vitamin A kwa watoto chini ya miezi sita hadi miaka mitano yalitolewa na kupatikana jumla ya watoto **251,074** sawa na asilimia **100.9** walipatiwa matone ya Vitamini A kwa Unguja na Pemba. Idadi hii ni kubwa ukilinganisha na kipindi kama hiki mwaka 2021/2022 ambapo jumla ya watoto **155,183** sawa na asilimia **67** walipatiwa matone ya Vitamin A kwa Unguja na Pemba. Mafanikio haya yamechangiwa na mashirikiano makubwa kutoka sekta mbali mbali za Serikali na binafsi hasa Masheha na wahudumu wa Afya wa kujitolea (CHVs).

38. **Mheshimiwa Spika,** Katika hatua ya kupunguza tatizo la upungufu wa damu kwa mama wajawazito, ufuatiliaji na utoaji wa elimu umefanyika kwa upande wa Unguja na jumla ya mama wajazito **1,021** waliohudhuria kliniki za mama na mtoto walichunguzwa wingi wa damu kwenye vituo vya Afya vilivotembelewa ambavyo ni KMKM Kibweni, Sebleni, Fuoni, Bububu Jeshini, Kwamtipura, Mpendae, JKU, Tawakkal hospitali na SDA Meya. Kati ya mama hao **557** sawa na aslimia **54.5** walibainika kuwa na upungufu wa damu. Aidha, elimu inaendelea kutolewa kupitia kliniki zote ili kupunguza tatizo la upungufu wa damu wakati wa ujauzito.

## HUDUMA ZA MARADHI YASIYOAMBUKIZA

39. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kuimarisha uchunguzi na matibabu ya maradhi yasiyoambukiza kupitia hospitali, vituo vya afya na ngazi ya jamii. Juhudi zaidi zimeelekezwa katika kuongeza uelewa katika ngazi ya jamii juu ya maradhi haya na vichocheo

vyake. Jumla ya wanawake **725** wamechunguzwa saratani ya matiti kupitia kampeni maalum za jamii, kati ya hao, wanawake **124** wamegunduliwa na uvimbe wa matiti, **50** walipewa rufaa kwenda Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa ajili ya uchunguzi na wanne (4) walifanyiwa upasuaji wa matiti. Aidha, Wizara inaendelea kusajili wagonjwa wa saratani kwa kuweka taarifa zao katika rejista maalum la wagonjwa wa saratani ambapo hadi sasa jumla ya wagonjwa **360** wameorodheshwa katika rejista hilo.

40. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha wananchi wanaendelea kupatiwa huduma ya maradhi yasiyoambukiza, jumla ya watu **2,800** wamefanyiwa uchunguzi wa maradhi mbali mbali yasiyoambukiza katika mabonanza yaliyofanyika katika ngazi ya jamii. Jumla ya wagojwa **201** waligundulika na hatari ya kupata kisukari, **35** waligundulika na kisukari, **150** walikuwa na uzito mdogo, **268** walikuwa na uzito uliokithiri, **297** waligundulika na hatari ya kupata shinikizo la damu na **47** wana tatizo la shinikizo la damu. Sambamba na zoezi hilo lililofanywa katika jamii, jumla ya wauguzi **251** walifanyiwa uchunguzi katika siku ya Kisukari Duniani. Katika uchunguzi huo, wauguzi **15** waligundulika na ugonjwa wa kisukari, wauguzi **30** walikutwa na sindikizo la damu, wauguzi **65** walikuwa na uzito mkubwa na **76** walikuwa na unene uliokithiri. Jumla ya vituo vya afya **46** vya daraja la pili (30 Unguja 16 Pemba) na Hospitali 8 ambazo ni Mnazimmoja, Makunduchi na Kivunge kwa Unguja na Abdalla Mzee, Vitongoji, Chakechake, Micheweni na Wete kwa Pemba walipatiwa mafunzo ya dalili za maradhi yasiyo ya kuambukiza ili kusaidia kuwatambua wagonjwa na kuwahimiza kuhudhuria kwenye vituo vya afya na hospitali.

**HUDUMA YA UFUATILIAJI WA MIENENDO YA MARADHI**

41. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Afya kupitia Kitengo chake cha ufuatiliaji wa mienendo ya maradhi inaendelea kufatilia maradhi ambayo yanayotolewa taarifa zake kila wiki kutoka katika vituo vya afya na hospitali kupitia mfumo wa kukusanyia taarifa za Afya (DHIS2), kwa kipindi cha mwezi wa Julai 2022 hadi Machi 2023, jumla ya visa 172,838 vya maradhi mbali mbali (kuharisha, malaria, kuharisha damu, homa ya matumbo (typhoid), kutafunwa na mnyama, tete kuanga, homa ya mapafu (nimonia)) viliripotiwa.

42. **Mheshimiwa Spika,** Taarifa za magonjwa hayo zinaonyesha ugonjwa wa kuharisha ndio unaongoza katika jamii kulinganisha na maradhi mengine ambapo jumla ya visa **48,726** sawa na asilimia **28** ikifuatiwa homa ya mapafu (nimonia) **32,027** sawa na asilimia **19**. Kwa upande wa ufuatiliaji wa matukio yanayohusiana na afya kupitia wahudumu wa afya wa kujitolea (CHVs), jumla ya matukio **84** ya ugonjwa wa surua yaliripotiwa na kufuatiliwa kutoka kwenye jamii. Aidha, nchi yetu ilikumbwa na mripuko wa ugonjwa wa surua ambapo jumla ya visa **2,245** vimeripotiwa pamoja na vifo **18**. Wilaya zilizoathirika zaidi na ugonjwa huo ni Magharibi A (**581)** sawa na asilimia **30**, ikifuatiwa na Magharibi B (**405)** sawa na asilimia **18** na Mjini **(271)** asilimia **13** kwa upande wa Unguja na kwa upande wa Pemba, Wilaya iliyoathirika zaidi ni Chake chake **292** asilimia **14**.

**43. Mheshimiwa Spika,** Katika jitihada za kukabiliana na janga la UVIKO-19 Wizara bado inaendelea kufuatilia washukiwa wote wa ugonjwa huo kuwafanyia vipimo vya haraka katika vituo vyote vya Afya Unguja na Pemba. Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, jumla ya watu **15,875** (washukiwa 7,125 na wasafiri 8,750) walipimwa UVIKO-19 kati yao **92** (washukiwa 68 na wasafiri 21) wamegundulika kuwa na maambukizi ya UVIKO-19 ambayo ni sawa na asilimia **0.6** na hakuna kifo kilichoripotiwa kwa kipindi hicho. Maambukizi ya ugonjwa wa UVIKO-19 yamepungua ukilinganisha na mwaka jana ambapo jumla ya watu **142** waliobanika kupata maambukizi ya UVIKO-19.

**HUDUMA ZA MARADHI YASIYOPEWA KIPAUMBELE**

**44. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia mwezi Machi 2023. Jumla ya wananchi **795** (Unguja **524** na Pemba **271**) walichunguzwa maradhi ya kichocho katika hospitali na vituo vya afya, kati ya hao **731** sawa na asilimia **91.9** waligundulika na maradhi hayo (Unguja **445** na Pemba **286**). Aidha waliochunguzwa maradhi ya matende walikua **79** kati yao **33** waliogundulika na vimelea vya ugonjwa huo na kupatiwa matibabu stahiki.

**45. Mheshimiwa Spika,** Wizara ilifaanya utafiti wa kuangalia vimelea vya maradhi ya matende katika shehia **23** (**15** Unguja na **8** Pemba) matokeo ya utafiti huo yalionyesha kuongezeka kwa maambukizi ya maradhi ya matende. Jumla ya sampuli **7,194** zilichunguzwa na matekeo yalionesha sampuli **67** sawa na asilimia **0.9** zilikua na maambukizi ya matende. Shehia zilizoongoza kuwa na

maambukizi mengi ni Kijini Makunduchi ambapo sampuli **16** ziligundulika kua na maambukizi hayo ikifatiwa na shehia ya Nungwi Kiungani ambapo sampuli **14** ziligundulika kua na maambukizi.

## HUDUMA ZA MSINGI ZA MATIBABU YA MACHO

**46. Mheshimiwa Spika,** Uchunguzi wa macho kwa jamii hasa vijijini unaendelea kutolewa, katika kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Machi 2023, Jumla ya watu **5,598** wakiwemo watoto 77 walifanyiwa uchunguzi wa macho na watu **2,967** walibainika kuwa na matatizo ya macho na walipatiwa matibabu hapo hapo. Kati ya hao watu **584** walipewa rufaa ya kuendelea na matibabu katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa upande wa Unguja na Hospitali ya Wete na Chake Chake kwa upande wa Pemba.

**47. Mheshimiwa Spika,** Katika kushirikiana na Madaktari bingwa wa Macho kutoka Tanzania Bara, Wizara iliendesha kambi za Upasuaji wa maradhi ya Mtoto wa jicho kwa watu wazima, kambi hizi zilifanyika katika hospitali kuu ya Mnazi Mmoja kwa upande wa Unguja na kwa upande Pemba ni Wete na Abdalla Mzee ambapo wagonjwa **226** walifanyiwa upasuaji.

**48. Mheshimiwa Spika,** Vile vile uchunguzi wa afya za macho kwa Wanafunzi ulifanyika katika Skuli mbali mbali za Unguja na Pemba ambapo jumla ya Wanafunzi **11,660** walichunguzwa afya zao za Macho kati yao jumla ya wanafunzi **103** walipatiwa matibabu pamoja na kupatiwa miwani.

## HUDUMA YA UTOAJI WA ELIMU YA AFYA

49. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 kitengo kimefanikiwa kuwafikia jumla ya wanajamii **149,996** na kuwapatia elimu ya afya kwa lengo la kujikinga na magonjwa, kuimarisha afya zao pamoja na kujiimarisha katika utumiaji wa huduma za afya na kujali afya zao, umuhimu wa chanjo ya surua, kinga ya Ebola, Udhalilishaji na unyanyasaji wa kijinsia kwa watoto, uhamasishaji juu ya uchanjaji wa chanjo ya Korona, Uchangiaji damu, Matumizi ya dawa za kutibu maji, Usafi wa mazingira, maradhi yasiyo ya kuambukiza, Uzazi wa mpango, Makuzi na malezi kwa watoto, Elimu kuhusu kichaa cha Mbwa na Saratani.

50. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuikinga jamii na maradhi ya kuambukiza na yasiyoambukiza, Elimu ya afya ndio msingi mkubwa wa kuwa na jamii yenye Kinga dhidi ya magonjwa mbali mbali, kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Elimu ya Afya ilitolewa kwa njia mbali mbali ambapo Skuli 150 Unguja na Pemba zilifikiwa kupatiwa elimu ya afya. Jumla ya wanafunzi **8,220** walipatiwa elimu ya afya juu ya kujikinga na magonjwa mbalimbali kama magonjwa ya Macho, Afya ya Kinywa, Afya ya Meno, Usafi wa Mazingira, Maradhi ya Kipindupindu, Maradhi ya Miripuko na Unyanyasaji wa Kijinsia.

51. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuendeleza utoaji wa elimu ya afya kwa njia tofauti kwa Shehia zote za Unguja na Pemba jumla ya "posters" **44,000** na vipeperushi **222,000** vilitolewa na kusambazwa kwenye jamii kwa ajili ya kuongeza uelewa wa

magonjwa mbalimbali pamoja na afya ya uzazi, chanjo za watoto na Korona kwa watu wazima. Aidha, kitengo kinaendelea kutoa elimu ya afya kwa vyombo vya habari, ambapo jumla ya vipindi vya Redio **275** vimerushwa kupitia Redio Nuru FM, Adhana FM, Zenji FM, Kati FM, Mtegani, Tumbatu FM, Plus FM, ZBC, Micheweni, Mkoani na Joel FM na kwa upande wa Vipindi vya TV Jumla ya Vipindi 58 vimerushwa kupitia ZBC TV na ZCTV.

**HUDUMA ZA AFYA YA MAZINGIRA**

**52. Mheshimiwa Spika,** Katika jitihada za kumaliza Kipindupindu Zanzibar Wizara inahakikisha jamii inakunywa maji safi na salama ambapo Wizara imegawa vidonge **361,950** vya dawa za kutibu maji katika shehia **46** zilizobainika kuwa na shida ya upatikanaji wa maji kutoka Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA). Aidha, jumla ya watu **653,750** walipatiwa dawa za kutibu maji hayo kutoka katika Shehia za Wilaya ya Mjini shehia tisa, Magharibi 'A' shehia **11** na Magharibi 'B' shehia **13** kwa Unguja na kwa upande wa Pemba Wete shehia **11** na Micheweni shehia **10**. Vilevile, jumla ya sampuli **49** za maji ya kunywa zimechunguzwa ambapo matokeo ya sampuli hizo yanaonesha sampuli **11** zina vimelea vinavyoweza kusababisha magonjwa ya miripuko ikiwemo kuharisha.

**53. Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha matumizi sahihi ya vyoo vilivyo bora, Wizara imefanya tathmini ya uhakiki wa nyumba zenye vyoo Unguja na Pemba ambapo jumla nyumba **900** kutoka shehia 182 zilifikiwa na matokea ya tathmini hiyo inaonyesha

asilimia **88** ya nyumba hizo wanatumia vyoo vilivyo bora. Aidha asilimia **12** nyumba zisizo na vyoo bora zinatarajiwa kupatiwa vyoo vilivyo bora aina ya SATO-PAN. Sambamba na hilo Wizara iko kwenye hatua za mwisho ya upatikanaji wa eneo maalumu la kuchomea taka zinazotoka hospitali katika eneo la Kibele.

**HUDUMA ZA AFYA BANDARINI**

54. **Mheshimiwa Spika,** Kupitia utowaji wa huduma hizi jumla ya wageni **462,222** waliingia nchini, Wasafiri **299,805** walitumia usafiri wa baharini na **162,417** walitumia usafiri wa anga, wasafiri wote walifanyiwa uchunguzi na ufuatiliaji. Katika uchunguzi huo hakukua na msafiri yoyote yule aliyeripotiwa kuwa na maradhi ya kuambukiza. Aidha, jumla ya maiti 68 na wagonjwa 148 walipitishwa na kukaguliwa kwa upande wa bandarini na uwanja wa ndege, Kati ya hao waliosafirishwa jumla ya wagonjwa wanne (4) walibainika na dalili za Korona na kupelekwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa hatua zaidi. Aidha, katika utoaji wa Chanjo dhidi ya kinga ya maradhi, jumla ya wasafiri wa nje ya nchi **824** walipatiwa chanjo za wasafiri ikiwemo chanjo ya homa ya manjano 774 na homa ya Ini ‘B’ 50.

55. **Mheshimiwa Spika,** Jumla ya kontena 23 zikiwemo za Nguo, Televisheni, Viatu na Majokofu zilizoingia nchini zimekaguliwa na kufanyiwa ufukizaji. Aidha, Wizara kupitia kituo kilichopo Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume imefanya uhakiki wa vyeti **16,002** vya Korona kwa wasafiri, ambapo jumla ya vyeti

**14,450** sawa na asilimia (**90.3**) vilikuwa vyeti halali na 202 sawa na asilimia **1.3** viligundulika kuwa vyeti bandia. Wahusika wa vyeti bandia wamefikishwa kwenye vyombo vya sheria.

**HUDUMA YA AFYA YA WAFANYAKAZI**

**56. Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha afya za Wafanyakazi zipo bora, Jumla ya wafanyakazi **36,998** kutoka taasisi mbali mbali za Serikali na Binafsi, Wanafunzi, Wafanya Biashara za Vyakula, Wafanyakazi Nje ya Nchi, Madereva wamepatiwa huduma hii. Kati ya hao jumla ya wafanyakazi wapatao **3,902** wameonekana kuwa na matatizo ya kiafya kama vile UTI **1,726**, Shindikizo la Damu **119**, Homa ya ini "B" **7**, Homa ya Ini C **15**, Maradhi ya ngozi **405**, Pumu **188**, Kisukari **29**, Ajali Kazini **29** na Uoni hafifu **807**. Wote waliobainika kuwa na matatizo walipatiwa ushauri wa kiafya na matibabu stahiki.

**57. Mheshimiwa Spika,** Jumla ya maeneo ya kazi 21 yalifanyiwa ukaguzi kwa lengo la kuhakikisha usalama na Afya kazini unazingatiwa sambamba na kuwalinda wafanyakazi katika maeneo yao ya kazi. Ukaguzi huu umejumuisha maeneo mbali mbali ya sekta za Serikali na binafsi. Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 maeneo yaliyofikiwa yakiwemo Skuli, Viwanda vitatu, Miradi ya Ujenzi wa hospitali za Wilaya mbili na Mkoa moja, Hoteli za kitalii tisa na Mikahawa saba. Changamoto zilizobainika ziliwasilishwa kwa wahusika kwa hatua stahiki. Ukaguzi huu ulifanyika sambamba na utoaji wa elimu ya afya na usalama mahali pa kazi.

## HUDUMA ZA AFYA YA MSINGI YA AKILI

58. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutoa huduma za afya ya msingi ya akili katika jamii pamoja na kusimamia haki na ustawi wa watu wenye matatizo ya afya ya akili. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 jumla ya wagonjwa wapya **754** walisajiliwa na kupatiwa huduma katika hospitali ya wagonjwa wa akili Kidongochekundu. Aidha, kwa kipindi hicho wagonjwa **438** walilazwa. Katika kuimarisha huduma za dawati rafiki jumla ya wateja wapya **253** wamesajiliwa na wateja **436** wanaendelea na huduma. Vile vile wagonjwa **91** wamepona na kuendelea na shughuli zao za kijamii na wagonjwa **12** walipatiwa rufaa kuendelea na matibabu zaidi katika hospitali wa wagonjwa wa akili Kidongochekundu.

59. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Pemba, Wizara imeendelea kuratibu shughuli za afya ya akili, ikiwa ni kusimamia haki na ustawi wa watu wenye matatizo ya afya ya akili nchini. Huduma za Afya ya Msingi ya Akili zimeendelea kutolewa katika hospitali 2 ambazo ni Hospitali ya Abdalla Mzee Mkoani na Hospitali ya Wete, ambapo katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 jumla wagonjwa **5,297** walipatiwa huduma za afya ya akili.

## HUDUMA ZA BARAZA LA WATAALAMU WA AFYA YA JAMII NA MAZINGIRA

60. **Mheshimiwa Spika,** Jukumu kuu la baraza hili ni kusimamia taaluma za kada ya Afya na Mazingira hapa Zanzibar ikiwemo pia kuwasajili na kuwapa leseni za kazi maofisa wa Afya ya Jamii na

Mazingira wanaofanyakazi Zanzibar, kwa kipindi cha Julai-2022 hadi Machi 2023 Baraza limefanya usajili na uhuwishaji wa leseni kwa Maafisa Afya **212** ambapo **105** walihuisha leseni zao na **107** walifanyiwa usajili kwa ngazi ya shahada ya uzamili, shahada ya kwanza na stashahada.

**61. Mheshimiwa Spika,** Katika muendelezo wa kimkakati kudumisha usafi wa Mazingira katika Jiji la Zanzibar, kwa kushirikiana na Mabaraza ya Manispaa ya Jiji la Zanzibar, Baraza lilifanya ukaguzi wa masoko likiwemo soko la Kibanda Maiti na Darajani. Lengo la ukaguzi huo ni kudumisha Usafi wa soko kiujumla na maeneo yanayohifadhiwa chakula, mama ntilie, Mabucha ya nyama na Uhifadhi wa taka ngumu na za maji.

**PROGRAMU YA HUDUMA ZA TIBA (PH0102)**

**62. Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa shughuli za Programu hii umegawika katika program mbili ndogo: Programu ya Huduma za Matibabu na Programu ya Huduma za Uchunguzi. Katika kipindi cha utekelezaji cha mwaka wa fedha 2022/ 2023, Programu ya Tiba ilipangiwa kutekeleza malengo yafuatayo: -

i. Kujenga hospitali mpya ya wagonjwa wa akili eneo la Kinyasini Pemba na hospitali ya Mkoa wa Kaskazini Unguja katika eneo la Mahonda

ii. Kujenga kituo cha damu salama Pemba

iii. Ukarabati mkubwa wa hospitali ya Wete

iv. Kuanzisha na kuhakikisha ngazi zote za utoaji wa huduma zinafuata miongozo na viwango vilivyothibitishwa na wizara ya afya katika utoaji wa huduma (national standards).

v. Kuanzisha utaratibu maalum wa utoaji wa huduma za afya kwa watalii

vi. Kuanzisha viwanda vya kutengeneza dawa na vifaa tiba

vii. Kuimarisha usimamizi katika uhifadhi na utumiaji wa dawa na vifaa tiba katika hospitali na vituo vya afya

viii. Ununuzi wa vifaa vya maabara ya Wakala wa Chakula na Dawa

ix. Kuanzisha vyama vya kitaaluma ‘’professional associations’’ ikiwemo wafamasia, wataalamu wa ubongo na uti wa mgongo, huduma za dharura, magonjwa ya kinamama na watoto, afya ya akili na nvenginezo

x. Kuimarisha mashirikiano na vyuo vikuu vya ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kusimamia miongozo ya utoaji huduma na mafunzo endelevu kwa wafanyakazi

xi. Kubadilisha mfumo wa utoaji wa huduma katika ngazi zote

xii. Kuanzisha ‘Center of Excellence for superspecialized medical services’ kwa ajili ya matibabu ya macho, mifupa na ajali (traumatology), saratani, uti wa mgongo na ubongo, moyo na meno.

63. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Fungu (PH0102), jumla ya shilingi **90,490,626,000/-** ambapo shilingi **86,911,126,000/-** kwa ajili ya huduma za matibabu na shilingi **3,579,500,000/-** kwa huduma za uchunguzi. Hadi kufikia Machi 2023 Programu hii iliingiziwa kiasi cha shilingi **25,622,083,073/-** sawa na asilimia **28.3**, kati ya hizo shilingi **20,713,694,309** zilitolewa kwa ajili ya huduma za matibabu na shilingi **4,908,388,764/-** kwa ajili ya huduma za uchunguzi.

## PROGRAMU NDOGO YA HUDUMA ZA MATIBABU

64. **Mheshimiwa Spika,** Huduma za matibabu ya Wagonjwa wa nje (Outpatient) na wagonjwa wa kulazwa (inpatient) zinaendelea kutolewa katika hospitali za rufaa ya Mnazimoja, Mkoa, Wilaya, hospitali maalumu za binafsi. Jumla ya mahudhurio ya wagonjwa wa nje ni **469,122** kwa wagonjwa waliolazwa kwa sababu ya matatizo ya maradhi mbali mbali ni **51,674** Aidha wagonjwa **2,643** wamefariki dunia, Mwenyezi Mungu awalaze malali pema peponi. Vile vile wazazi **57,849** walijifungua kwa njia ya kawaida na wazazi **52,488** walijifungua kwa njia ya upasuaji **6,684**. Aidha, vichanga viliozaliwa hai **52,610** na vichanga vilivyofariki **1,254.** Aidha mahudhurio ya **238,272** wameripotiwa katika klinik za maradhi maalumu kwa Unguja na Pemba kliniki hizo zinajumuisha magonjwa ya Kisukari, Shinikizo la damu, moyo na mengineyo. **Kiambatisho nambari 3 b, c na d** kinafafanua.

65. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na idadi kubwa ya watu ambao wamepatiwa huduma za matibabu hapa hapa Zanzibar, kuna baadhi ya wagonjwa ambao hupatiwa matibabu nje ya nchi

kwa ajili ya matibabu ya rufaa kwa vile maradhi yao yalihitaji vifaa vya uchunguzi na utaalamu zaidi. Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 jumla ya wagonjwa **402** walisafirishwa Tanzania bara na nje ya nchi kama ifuatavyo; Tasisi ya Mifupa ya Hospital ya Taifa Muhimbili (MOI) **63**, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili **165**, Tasisi ya magojwa ya moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) **101** na Ocean Road **11**. India Miot **62**.

**HUDUMA ZA USHIRIKIANO WA AFYA KIMATAIFA**

**66. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeona kuna umuhimu mkubwa wa kuanzisha Kitengo cha Ushirikiano wa Afya Kimataifa ili kukuza mashirikiano kwa ajili ya kutoa huduma za afya kwa jamii hususani kwa magojwa ya kibingwa. Kitengo hichi kimeanza kazi mwaka 2022 na tayari tumeshafanikiwa kukutana na madaktari bingwa kutoka katika nchi za Kuwait, Holand, UK, Israel na Marekani nchi hizi zote zimeweza kutoa huduma mbali mbali za kitibabu kupitia kambi katika maeneo tofauti ya Unguja na Pemba. Jumla ya kambi sita zilifanyika katika kutibu maradhi mbali mbali yakiwemo magonjwa ya akina Mama na jumla ya akina Mama watatu walichunguzwa na kufanyiwa upasuaji, matatizo ya mifupa ambapo jumla ya wagonjwa **17** walichunguzwa na kufanyiwa upasuaji, magonjwa ya moyo kwa watoto ambapo jumla ya watoto **33** walichunguzwa. Pia kwa upande wa matatizo ya macho jumla wa wagojwa **1,110** walichunguzwa na wagonjwa **487** walipatiwa miwani. Aidha kupitia kambi ya Madaktari bingwa kutoka Egypt jumla ya wagonjwa **298** walifanyiwa upasuaji kwa matatizo ya kina mama, mifupa, upasuaji wa kawaida na matatizo ya mkojo. **Kiambatisho nambari 4** kinafafanua.

## HUDUMA ZA DAMU SALAMA

**67. Mheshimiwa Spika,** Wizara imekusanya uniti za damu **11,898** kutoka kwa wachangiaji wa hiari kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023. Hii ni sawa na asilimia **59** ambapo lengo lilopangwa ni kukusanya uniti 20,000 za damu. Makusanyo ya uniti **11,898** za damu zilifanyiwa mazalio yaliozalisha unit **21,407**. Jumla ya uniti **14,441** sawa na asilimia 34 kutoka kwenye maombi ya uniti **42,139**, zilisambazwa katika hospitali kwa matumizi mbali mbali. Ukusanyaji huu ulifanikishwa kupitia mabonanza ya uchangiaji damu yaliyoendelea kufanyika katika maeneo mbali mbali.

## HUDUMA ZA MKONO KWA MKONO (ONE STOP CENTRE)

**68. Mheshimiwa Spika,** Katika sehemu hii ya huduma za makosa ya udhalilishaji wa ngono na kijinsia zinahitajika juhudi za makusudi kwa ajili ya kuliondoa tatizo hili kubwa lililoikumba jamii yetu, taarifa zilizoripotiwa kutoka julai 2022 hadi kufikia machi 2023, Jumla ya idadi ya matukio **1,217** yaliyoripotiwa kwa matukio tofauti yakiwemo Jaribio la kubaka **11**, kubaka **382**, kubaka na kulawiti **145**, Jaribio la kulawitiwa **10**, Kulawiti **135**, kukashifu **108**, udhalilishaji kimwili **209**, udhalilishaji kijinsia **103**, ujauzito **32** na kutelekezwa **82**.

## HUDUMA ZA BODI NA MABARAZA YA KITAALUMA

### HUDUMA ZA USHAURI HOSPITAL BINAFSI

**69. Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi, moja ya kazi yake kubwa ni kufanya ukaguzi wa vituo na hospitali binafsi ili kuona vigezo vilivyowekwa vinatimizwa na kufuatwa kwa mujibu wa sheria nambari 4 ya mwaka 1994. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2023, jumla ya dispensari **62** na hospitali 4 zimekaguliwa. Aidha, jumla ya maombi **9** ya kufungua vituo vipya yalipokelewa na kupatiwa usajili baada ya kukidhi vigezo. Vituo hivyo ni Cooldent Dental Klinik, Tahsiin dispensary, Ihsaan Dispensary, Agakhan Polyclinic, Bapumia Specilized Medical Clinic, Amani First aid clinic, Emerld First aid clinic, AMS Medical centre na Dr. Lii Dispensary.

### HUDUMA ZA BARAZA LA WATAALAMU WA MAABARA ZA TIBA

**70. Mheshimiwa Spika,** Baraza hili limeanziswa chini ya sheria nambari 10 ya mwaka 2020, ambalo linajukumu la kusimamia wataalamu na kudhibiti taaluma ya maabara pamoja na masuala mengine yanayofanana na hayo. Hadi sasaBaraza limesajili jumla ya wataalamu **462** (Unguja 416 na 43 kwa Pemba). Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, jumla ya wataalamu 361 waliwasilisha maombi yao ya usajili na kupatiwa usajili  kama sheria inavyoeleza.

## HUDUMA YA BARAZA LA TIBA ASILI NA TIBA MBADALA

**71.** **Mheshimiwa Spika,** Sheria namba 8 ya mwaka 2008 ya Baraza la Tiba Asili na Tiba mbadala limefanikiwa kusajili Kliniki **48**, Kliniki za tiba mbadala **5**, Maduka ya dawa asili 207, Waganga wa tiba asili **524**, wasaidizi waganga **176**, pamoja na ghala **mbili** za dawa asili. Watendaji wa Baraza wanaendelea kutoa elimu kwa jamii kupitia vyombo vya Habari juu ya matumizi sahihi ya dawa asili, pamoja na kuwahamasisha waganga wa wauzaji dawa za asili ili waweze kujisajili kwa lengo la kurasimisha huduma zao wanazozitoa kwa wananchi. Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Baraza limeweza kutoa vibali **72** vya usafirishaji wa dawa nje ya nchi (Export permit) na vibali **7** vya uingizaji wa dawa nchini (Import Permit).

**72.** **Mheshimiwa Spika,** Pamoja na hayo, Baraza la tiba asili kwa kushirikiana na Jeshi la polisi linaendeleza juhudi zake za kufanya Ukaguzi ili kupambana na wimbi la waganga wanaojilabu na wanaokiuka Sheria na miongozo ya tiba kwa kuuza dawa kiholela kwenye maeneo yenye mikusanyiko ya watu kama vile masokoni na misikitini. Lengo ni kuhakikisha kuwa wadau wa tiba asili wanatoa huduma zao kwa weledi na kuzingatia misingi ya Sheria, Kanuni na Miongozo. Aidha jumla ya vituo vya tiba asili **154** ikijumuisha watabibu wa tiba asili **37**, kliniki za tiba asili saba, maduka ya dawa asili **110**. Ukaguzi huo ulibaini mapungufu ya usajili na kupelekea jumla ya maduka **16** kufungwa kwa muda hadi baada ya kukamilisha taratibu za usajili kwa mujibu wa sheria.

## HUDUMA ZA BARAZA LA MADAKTARI

73. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 Baraza la Madaktari limesajili madaktari Bingwa wazalendo **20** na wakigeni 3, Madaktari wa kawaida wazalendo 80 na wakigeni 2, Daktari wa meno mzalendo mmoja na wakigeni mmoja, Daktari wasaidizi wazalendo wanne, Afisa tabibu wazalendo **195** na Afisa tabibu kinywa **24**. Kwa upande wa waliohuisha leseni Madaktari bingwa wazalendo **86** na wakigeni saba, Daktari wa kawaida wazalendo **165** na wakigeni **10**, Daktari wa meno wazalendo **11** na wakigeni **2**, Daktari wasaidizi wazalendo **42**, Daktari wasaidizi wa 2, Afisa tabibu wazalendo **348** na Afisa Tabibu Kinywa **50**.

## HUDUMA ZA BARAZA LA WAUGUZI NA WAKUNGA

74. **Mheshimiwa Spika,** Hadi sasa Baraza limefanikiwa kusajili wauguzi na wakunga **2,773** Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 Baraza la Wauguzi na Wakunga limesajili na kuwapa leseni wauguzi wapya **234**. Aidha, wauguzi wanaohuisha leseni **494** kati ya hao **344** Unguja na **150** Pemba. Katika kuhakikisha huduma za uuguzi zinatolewa katika kiwango kilicho bora, Baraza kwa kushirikiana na Muuguzi Mkuu limefanya ziara katika hospitali za Abdalla Mzee, Wete na Chake Chake ambapo lengo la ziara hizo ni kuangalia jinsi huduma za uuguzi zinavyotolewa na pia kuona changamoto zinazowakabili wauuguzi katika utoaji wa huduma. Kwa upande wa usimamizi wa maadili ya wauguzi na wakunga jumla ya kesi **mbili** ziliripotiwa na Baraza lilichukua hatua kulingana na utekelezaji wa sheria namba 5 ya mwaka 2014 ya Baraza la Wauguzi na Wakunga.

## HUDUMA YA UPATIKANAJI, UHIFADHI, USAMBAZAJI WA DAWA NA VIFAA TIBA

## OFISI YA MFAMASIA MKUU WA SERIKALI

**75. Mheshimiwa Spika,** Ofisi hii ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa dawa muhimu, vifaa tiba pamoja na kusimamia matumizi sahihi ya dawa. Katika kulifikia lengo hili, Ofisi ya Mfamasia Mkuu imepewa dhamana ya kufanya maoteo ya dawa (quantification) pamoja na kuratibu ununuzi wa dawa na vifaa tiba, kufanya ukaguzi kwenye Hospitali na Vituo vya afya ili kuhakikisha utunzaji bora na utumiaji sahihi wa dawa, pia kusimamia mfumo wa kielektroniki (eLMIS) kuripoti matumizi na uombaji wa Dawa na Vifaa Tiba kwenye Hospitali na Vituo vya Afya. Aidha, wizara imefanya zoezi la maoteo ya Dawa na Vifaa Tiba (Quantification of Health commodities) kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kwa lengo la kupata makisio sahihi ya dawa na vifaa tiba vitakavyo hitajika kwa mwaka. Pia, zoezi la kufanya makisio ya Dawa za uzazi wa mpango na Dawa za kuokoa maisha kwa mama na mtoto kwa kipindi cha mwaka mmoja 2023/2024 limefanyika.

**76. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi ya Mfamasia Mkuu ilitengewa shilingi **31,145,570,000/-** kwa ajili ya kununua dawa na vifaa tiba. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2023, Jumla ya shilingi **6,850,000,000/=** sawa na asilimia 23 zimetolewa kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba. Kati ya fedha hizo, Tsh. **2,460,000,000/=** zilitumika kwa ajili ya ununuzi wa Dawa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na Tsh. **4,390,000,000/=** kwa ajili ya Hospitali za Mkoa, Wilaya pamoja na vituo vya afya Unguja na

Pemba. Sambamba na hilo jumla ya hospitali mpya tano na vituo vya Afya **39** zilifanyiwa ukaguzi kwa lengo la kuangalia matayarisho ya sehemu zitakazotumika kutolea na kuhifadhia dawa. Katika ukaguzi huo Ofisi ya Mfamasia Mkuu ilikuta mapungufu mbali mbali kwenye maeneo ya kutolea na kuhifadhia dawa yakiwemo udogo wa ghala za kuhifadhia dawa, kukosekana kwa "shelves na palate" pamoja na samani.

77. **Mheshimiwa Spika,** Zoezi la kufanya tathmini itakayopelekea upatikanaji wa Mwongozo wa Mnyororo wa ugavi na usambazaji wa Dawa na vifaa tiba wakati wa dharura "Assessment of Emergency Supply Chain Operation" lilifanyika. Tathmini hii itasaidia kuainisha maeneo muhimu yatakayohitajika kuandaliwa kwenye Mwongozo huo ambao kukamilika kwake kutatoa maelekezo ya utaratibu mzima utakaotumika kutoa huduma za dawa na vifaa pamoja na majukumu ya kila mdau. Aidha, Wizara inaandaa miongozo mbalimbali ikiwemo muongozo wa utoaji wa dawa na vifaa tiba kutoka kwa wahisani na muongozo wa matibabu kwa watoto ambayo itarahisisha upatikanaji, usambazaji na utumiaji wa dawa pamoja na kutatua changamoto zitakazojitokeza.

## IDARA YA BOHARI KUU YA MADAWA

78. **Mheshimiwa Spika,** Jumla ya kiasi cha fedha shilingi **280,295,625/=** zilipangwa kwa kipindi cha Julai 2022 Machi 2023 kutoka mfuko mkuu wa fedha za Serikali kwa upande wa Bohari kuu ya dawa

Unguja. Jumla ya fedha shilingi **26,000,000/=** ambayo ni sawa na asilimia tisa ya fedha zilipatikana. Aidha, kwa upande wa Bohari Kuu ya Dawa Pemba jumla ya kiasi cha fedha shilingi **171,679,400/=** zilipangwa kutoka mfuko mkuu wa fedha za Serikali, jumla ya shilingi **43,667,260/=** sawa na asilimia **25** ya fedha zilipatikana. Aidha Bohari kuu ya Dawa ilipokea shilingi **199,472,875/=** kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa ajili ya kuchangia shughuli za uhifadhi na usambazaji.

**79.** **Mheshimiwa Spika,** jumla ya maeneo **201** (distribution points) ambayo Bohari kuu ya Madawa inasambaza dawa na vifaa vya utibabu vikiwemo visiwa vidogo vidogo sita (1 Unguja na 5 Pemba). Idadi hii inajumuisha vituo vya afya **161**, hospitali **9**, vituo na hospital **14** zinazomilikiwa na vikosi vya ulinzi pamoja na hospitali binafsi zinazotoa huduma za Mama na Mtoto (RCH) **13**, huduma ya UKIMWI **3** na huduma ya damu salama **2** (1-Unguja na 1-Pemba). Aidha katika kuimarisha upatikanaji wa dawa Bohari Kuu ya Dawa imetoka kwenye usambazaji wa dawa kwa kila miezi mitatu na zoezi hilo hufanyika kwa kila mwezi ili kupunguza changamoto ya upungufu wa madawa katika vituo vya afya. Katika kuimarisha utoaji wa huduma kwa upande wa Bohari kuu ya dawa Pemba tayari wanatumia mfumo wa uhifadhi na usambazaji wa madawa na tayari wamejengewa uwezo wa kutumia mfumo huo. Katika hatua nyengine wazabuni wanapeleka dawa moja kwa moja kwa upande wa Pemba.

**PROGARAMU NDOGO YA HUDUMA ZA UCHUNGUZI (SH030202)**

**HUDUMA ZA WAKALA WA CHAKULA NA DAWA**

**80. Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Chakula na Dawa ni Taasisi yenye jukumu la kusimamia na kudhibiti usalama, ubora na ufanisi wa Chakula, Dawa, Vipodozi, Vifaa Tiba na Vitendanishi na inafanya kazi zake kwa mujibu wa Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi sheria nambari 2 ya mwaka 2006 na marekebisho yake ya Sheria nambari 3 ya mwaka 2017.

**81. Mheshimiwa Spika,** Wakala katika utekelezaji wa majukumu yake ya msingi hadi kufikia mwezi wa Machi 2023 ilikagua jumla ya maeneo ya biashara **4,400** kati ya maeneo **4,418** yaliopangwa kukaguliwa sawa na asilimia **99.5**, yakiwemo maeneo ya Chakula **3,412** (Unguja 1,575 na Pemba 1,837), Maduka ya dawa **720** (Unguja 593 na Pemba 127), Maduka ya Vipodozi **250** (Unguja 123 Pemba 127), na Maduka ya vifaa tiba **18** kwa Unguja. Aidha, kwa upande wa usajili wa maeneo, jumla ya maeneo **698** (Unguja 537 na Pemba 161) yakiwemo maeneo chakula **606**, Maduka ya dawa **32**, Maduka ya vifaa vya utibabu **16** na maduka ya Vipodozi **44** sawa na asilimia **50** kati ya maeneo **1,405** iliyojipangia kuyasajili. Vilevile, jumla ya maombi ya usajili wa bidhaa **96** yalipokelewa ambapo bidhaa **25** zikiwemo za Chakula 7, Dawa **2**, Vipodozi **10** na Vifaa vya Utibabu 6 zimesajiliwa baada ya kufanyiwa tathmini na kukidhi viwango vya kusajiliwa.

**82. Mheshimiwa Spika,** Wakala hadi kufikia Machi 2023 kupitia maabara yake ilichunguza jumla ya sampuli 1,**242** kati ya sampuli **2,800** sawa na asilimia **44** zikiwemo Chakula **1,158** Dawa **8**,

Vipodozi **69** na Vifaa Tiba **7** zilifanyiwa uchunguzi ambapo Sampuli **111** (Chakula **107**, Dawa 1 na Vipodozi 3) hazikufikia viwango vilivyowekwa na kugundulika hazifai kwa matumizi ya binaadamu.

## HUDUMA ZA WAKALA WA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI

**83. Mheshimiwa Spika,** Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Zanzibar imegawika katika tasisi kuu tano ambazo ndizo zinazoendesha na kutekeleza shughuli zote za Taasisi. Idara zenyewe ni Idara ya Utawala na rasilimali watu, Mipango na Tafiti, Idara ya Kemikali na Mazingira, Idara ya Chakula na dawa, Idara ya Sayansi ya Makosa ya Jinai pamoja na Idara ya Kusimamia Ubora.

**84. Mheshimiwa Spika,** kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 Wakala imefanikiwa kupokea sampuli **65** kwa ajili ya uchunguzi. Aidha katika hatua nyengine Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ilifanikiwa kutoa vibali **1,104** vya uingizaji, usafirishaji na utoaji wa kemikali, na ilifanikiwa kusajili maeneo **21** ya kuhifadhia kemikali, maeneo **50** pia yalibadili hati za usajili (renew) na vilevile imefanikiwa kufanya ukaguzi katika maeneo **87** yanayohifadhi kemikali.

**85. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Jumla ya vielelezo **457** vilipokelewa kutoka sehemu mbali mbali kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi, vielelezo hivyo vilikuwa ni dawa za kulevya **78**, Pombe za kienyeji **22**, Bangi **147**, Mikojo **56**, Sumu **17**, Damu **18**, Mafuta ya petrol kielelezo kimoja, Mirungi vielelezo

vitatu, Shisha kielelezo kimoja na vinasaba (DNA) **114**. Aidha, kwa upande wa Chakula na Dawa Wakala ilifanikiwa kupokea sampuli **1,088** kwa ajili ya uchunguzi, kati ya hizo jumla ya sampuli **919** zilikuwa za chakula na sampuli **169** zilikuwa za dawa, uchunguzi wa sampuli hizo umeonyesha sampuli zote zilikuwa zinafaa kwa matumizi ya binaadamu.

**PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA (PH0103)**

**86. Mheshimiwa Spika,** programu hii inahusika na usimamizi wa rasilimali watu, rasilimali fedha, manunuzi, sheria na shughuli nyengine za uendeshaji wa Wizara. Aidha, ina jukumu la kuandaa na kusimamia sera, miongozo, mipango pamoja na kuratibu taarifa za afya.

**PROGRAMU NDOGO YA UTAWALA NA UENDESHAJI (SH010301)**

**87. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ilitenga kiasi cha shilingi **9,043,011,000/=** hadi kufikia Machi 2023 iliingiziwa na kutumia jumla ya shilingi **5,259,573,020/=** sawa na asilimia **58.1**.

**NGUVU KAZI YA SEKTA YA AFYA**

**88. Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha Wizara ina wafanyakazi wa kutosha katika kutoa huduma za afya Wizara imeajiri wafanyakazi **710** wakiwemo Madaktari **122**, Daktari wa Meno **13**, Wafamasia **30**, Wauguzi **264**, Maafisa Tabibu **60**, Maafisa Maabara **15**, Wafiziotherapia **21**, Afisa Afya Mazingira **37**, Afisa Ushauri Nasaha **29**, Afisa Tabibu Meno **34** na “Phamaceutical technician” **70**. Aidha, wafanyakazi **191** wamerudi kutoka masomoni

wakiwemo Wataalamu wa ganzi na usingizi **11**, Wataalam wa Maradhi ya akina mama **sita**, Wataalam wa maradhi ya watoto **wawili**, Wataalam wa maradhi ya Moyo **watatu**, Wauguzi **46**, Mtaalam wa Maradhi ya Macho **mmoja**, Wafamasia **watatu**, Wataalamu wa Mionzi **watatu** na Mtaalam wa Matatizo ya Mkojo **mmoja**. **Kiambatisho nambari 5** kinafafanua.

**89. Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha wafanyakazi wanatoa huduma kwa ufanisi Wizara katika kipindi cha mwaka 2022/2023 imewapeleka masomoni wafanyakazi **91** wa kada mbali mbali ndani na nje ya nchi (Wataalam wa maradhi ya watoto **10**, Wataalamu wa ganzi na usingizi wanne na Wataalamu wa Mionzi wanane) na kuifanya idadi yote ya wafanyakazi waliokuwepo masomoni kuwa **866**. Aidha, Wafanyakazi **75 wamestaafu** kwa mujibu wa sheria na wafanyakazi **sita** wamefariki dunia Mungu azilaze roho za marehemu peponi Amin.

**HUDUMA ZA AFYA KIDIGITALI**

**90. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Afya imeendelea na utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Miaka mitano wa Dijitali za Afya Zanzibar (Zanzibar Digital health Strategy 2020/2025) wenye lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za afya zenye usalama, usawa, ubora na ufanisi katika ngazi zote kwa kutumia teknolojia ya dijitali za afya.

**91. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara imeanza kutumia mfumo wa kielektroniki wa usajili wa wagonjwa "ZanEMR" ambao unatumika katika hospitali ya Mkoa Abdalla

Mzee, Hospitali za Wilaya za Chakechake, Wete, Micheweni na Vitongoji kwa upande wa Pemba; na upande wa Unguja ni Hospitali za Wilaya Kivunge, Makunduchi na Kitogani. Lengo la Wizara ni kutumia mfumo huo kwenye hospitali zote mpya zilizojengwa na kisha kuanzisha matumizi hayo kwenye vituo vya Afya vyote **168** vya ngazi ya msingi.

**92. Mheshimiwa Spika,** Katika kukabiliana na maradhi ya miripuko Wizara imeandaa mfumo wa kidijitali wa kufuatilia maradhi ya miripuko (Electronic Disease Surveillance and Response-eIDSR) unaompa uwezo Afisa mfatiliaji wa afya (Surveillance Officer) kufuatilia watu waliokutana na mgonjwa (contact tracing). Kwa kutumia mfumo huo watoa huduma wanauwezo wa kuwatambua wagonjwa na kuwahudumia, lakini pia husaidia kupunguza maambukizi na hatimae kuzuia kusambaa kwa magonjwa ya miripuko.

**93. Mheshimiwa Spika**, Uimarisha wa ubora wa taarifa Wizara imeandaa mfumo wa kuunganisha mifumo ya afya (Zanzibar Health Interoperability Layer) unaosaidia kubadilishana taarifa za afya (shared health records) kwa kutoa fursa mfumo mmoja kuupa taarifa mfumo mwengine na kutoa taarifa zikiwa sahihi badala ya kila mfumo kukusanya taarifa upya. Mfumo huo unawarahisishia watoa huduma kupata taarifa za uhakika na kuharakisha utoaji wa huduma.

**94. Mheshimiwa Spika,** Kuimarika kwa matumizi ya mifumo ya digitali katika kutoa huduma za afya huharakisha utoaji wa huduma kwa wagonjwa, kutunza kumbukumbu za wagojwa zinazosaidia muendelezo wa huduma zake, kupunguza matumizi mabaya ya dawa na vifaa tiba, kupima viwango vya watoa huduma na kukusanya taarifa za afya zenye uhakika na kutoa ripoti kwa wakati kwa ajili ya kufanya maamuzi ya kiafya.

**USIMAMIZI WA SHERIA**

**95. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeandaa Sheria mbali mbali za Afya ili kuenda sambamba na utoaji mzuri wa huduma za Afya ikiwemo Kuandaa Sheria ya Mfuko wa huduma za Afya kwa wote, ya mwaka 2023 ambayo **imeshapitishwa** na Baraza la Wawakilishi, Rasimu ya sheria ya Wakala wa Bohari imeshatayarishwa na muda mfupi inategemewa kupitishwa kuwa sheria. Katika hatua nyengine, rasimu ya kwanza ya Sheria ya Wataalamu wa dawa ambayo kwa sasa ipo katika hatua ya kupelekwa kwenye kikao cha Makatibu wakuu.

**96. Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha huduma za Afya zinaimarika na mazingira mazuri ya kutolea huduma yanapatikana. Wizara imeandaa Mikataba ya ujenzi wa hospitali kumi na moja (11) za Wilaya Unguja na Pemba ambapo hospitali 10 zimeshakamilika ujenzi wake na hospitali mbili kati ya hizo zimefunguliwa na tayari zinaendelea kutoa huduma ambazo ni Hospitali ya Kitogani na Hospitali ya Micheweni. Hata hivyo, kwa upande wa hospitali ya Mkoa iliyopo Lumumba tayari ujenzi wake kukamilika.

**PROGRAMU NDOGO YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI (SH010302)**

97. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 programu hii ilitengewa kiasi cha shilingi **1,449,227,000/-**, ambapo hadi kufika **Machi** 2023 iliingiziwa na kutumika jumla ya shilingi **551,322,017/-** sawa na asilimia **35.**

98. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha ufuatiliaji wa miongozo ya utoaji wa huduma za afya, Wizara iliandaa muongozo wa Kitita cha Utoaji wa Huduma za afya "Essential Health Care Package" ambao umeshakamilika na kuzinduliwa rasmi. Hatua inayoendelea ni kufuatilia utekelezaji wake kupitia mfumo mama wa Wizara (DHIS2). Aidha, viashiria na shabaha zake tayari vimeshaingizwa katika mfumo huo kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wake.

99. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kutayarisha taarifa mbali mbali za utekelezaji wa Wizara zikiwemo za mwaka "Annual Health Sector Performance Report", Ripoti za robo mwaka, Taarifa za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, Ripoti za Utekelezaji wa Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi, Ripoti ya utekelezaji wa Wizara kwa mwaka 2022/2023 pamoja na Hotuba ya Bajeti ya mwaka 2023/2024, ambayo leo ninaisoma mbele ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Taarifa nyengine zilizotayarishwa ni utekelezaji wa ilani na maagizo mbali mbali ya serikali, taarifa ya maendeleo ya **sekta** ya afya katika maadhimisho ya miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar na taarifa ya Wizara ya Afya katika hotuba ya Makamo wa Pili wa Rais.

**100. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea na zoezi la kusafisha takwimu za afya kwa lengo la kuimarisha ubora wa taarifa hizo ambazo zinatumika katika kufanya maamuzi mbali mbali ya kiafya kwa wakati.

**101. Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya zenye ubora, ukaguzi kwa hospitali na vituo vya afya ulifanyika, ambapo jumla ya hospitali **sita** (Unguja **tatu** na Pemba **tatu**) na vituo vya afya **96** (Unguja **50** na Pemba **46**) vilifanyiwa ukaguzi. Lengo la ukaguzi huo ni kuangalia ubora wa huduma zinazotolewa ikiwemo uwepo wa dawa, wafanyakazi na miundombinu ya kituo. Sambamba na hilo kwa Wizara imefanya usimamizi yakinifu "Supportive Supervision" katika hospitali na vituo vya afya **102** vilivyounganishwa katika mfumo wa ubora "Quality Plat forms" vilevile Wizara imekamilisha uandaaji wa kitita cha viwango vya msingi vya utoaji wa huduma za afya "basic standard of Health facilities" kwa lengo la kuimarisha ubora wa huduma za afya nchini.

**102. Mheshimiwa Spika,** Mafunzo juu ya matumizi ya taarifa za afya na uandishi wa ripoti yalifanyika ambapo jumla ya wafanyakazi **43** (Unguja **20** na Pemba **23**) walipatiwa mafunzo hayo kwa lengo la kuwajengea uwezo katika ufanyaji wao wa kazi zinazohusiana na ufuatiliaji na tathmini. Aidha, mkutano wa watafiti wa afya Tanzania "Tanzania Health Sumit" 2022 ulifanyika na jumla ya watafiti 12 kutoka Wizara ya Afya Zanzibar walishiriki mkutano huo na tafiti nne kutoka Zanzibar ziliwasilishwa katika mkutano

huo. Sambamba na hilo watafiti kutoka Zanzibar walipata bahati ya kubadilishana uzowefu na watafiti wengine kutoka Tanzania Bara na Duniani kwa ujumla, pia kupeana ujuzi na kupendekeza mashirikiano kwa maeneo wanayofanyia tafiti zao.

103. **Mheshimiwa Spika,** Mkutano wa 13 wa mapitio ya utekelezaji wa Sekta ya Afya umefanyika na kutoa maadhimio yafuatayo:- kuimarisha mfumo wa rufaa za wagonjwa wa ndani na nje ya nchi, kuanzisha mpango kinga wa zana na vifaa tiba, kuimarisha upatikanaji wa dawa muhimu kwa mama wajawazito, kuimarisha programu za uhamasishaji katika ngazi ya jamii, kuimarisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba, kuzingatia ugawaji wa bajeti kwa usawa na kuongeza idadi ya ajira ambazo zitasambazwa kwa mujibu wa mahitaji.

104. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha huduma za Afya zinapatikana kwa wote bila ubaguzi. Wizara, imeandaa Mpango Mkakati wa Kugharamia Huduma za Afya (Health Financing Strategy) ambao kwa sasa upo kwenye hatua ya kupitiwa na wadau ili kukusanya maoni.

105. **Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Uanzishwaji wa Mfuko wa Huduma za Afya imeshatiwa saini na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Aidha katika utekelezaji wa sheria hii Wizara imeanzisha Akaunti maalumu ambayo itawahudumia wasio na uwezo “Zanzibar Health Equity Account”.

106. **Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar ni Taasisi inayojitegemea ambayo imeanzishwa kwa **Sheria Nam. 1 ya mwaka 2023**. Malengo ya Taasisi hii ni kufikia upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wote, za uhakika na endelevu kwa wananchi na wakaazi wote wa Zanzibar na kuimarika kwa upatikanaji wa rasilimali fedha za kutosha na endelevu za kugharimia huduma za afya.

107. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 mfuko huo ulikadiriwa kutumia jumla ya shilingi **1,549,893,000/=** kupitia bajeti ya Serikali ya kazi za maendeleo kwa ajili ya kazi za awali za uanzishwaji wa mfuko. Hadi kufikia Machi 2023, ofisi ya uratibu imeweza kutekeleza kazi zifuatazo:

i. Kupitishwa kwa Sheria ya Mfuko wa Huduma za Afya Nam.1 ya 2023 na Baraza la Wawakilishi na kusainiwa na Mheshimiwa Rais tarehe 20 mwezi wa Machi 2023;

ii. Kukamilika kwa Rasimu ya Kanuni za Sheria ya Mfuko wa Huduma za Afya Nam.1 ya 2023;

iii. Kukamilika kwa uandikaji wa mfumo wa usimamizi wa kielektroniki wa Mfuko (Software requirements Specification - SRS);

iv. Kukamilika kwa "model" ya usajili na tathmini ya uchangiaji wa Sekta isiyorasmi;

v. Kukamilika kwa "Portal" ya Usajili wa Wanachama wa Mfuko

vi. Kukamilika kwa Muongozo wa Uendeshaji wa Shughuli za Mfuko (Standards Operating Procedures – SOP);

vii. Kupatikana Ofisi za Mfuko katika Jengo la Michenzani Mall;

viii. Kukamilika kwa Tathmini ya Uhai na Uendelevu wa Mfuko.

## TAASISI YA UTAFITI WA AFYA (ZAHRI)

**108. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Taasisi hii ilipangiwa kiasi cha shilingi **1,119,300,000/=** ambazo ni ruzuku kwa ajili ya matumizi mengineyo (shilingi **642,000,000**) na mishahara (shilingi **477,300,000**). Hadi kufikia Machi 2023 shilingi **68,000,000/=** sawa na asilimia **6.1** zimeingizwa kwa ajili ya matumizi mengineyo. Katika utekelezajiwa majukumu yake Taasisi imeanza utafiti unaohusiana na magonjwa ya figo na kisukari kwa mama wajawazito. Aidha, Taasisi ya Utafiti inaendelea kufanya mapitio ya matoleo ya tafiti "Research Proposals" kwa wadau wa afya na wanafunzi. Kwa kipindi cha Julai 2022 Machi 2023, Taasisi imepitia matoleo ya tafiti **109** kutoka kwa wanafunzi, miradi **26** na tafiti za haraka haraka nane.

## PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA WIZARA YA AFYA PEMBA (SH010303)

**109. Mheshimiwa Spika,** Program hii ilitengewa jumla ya Shilingi **13,014,833,000/=,** kati ya hizo, **Shilingi 12,651,527,000/=** Kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 363,306,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, jumla ya shilingi **15,455,399,022/=** zilipatikana, kati ya hizo **15,295,470,272** kwa ajili ya malipo ya mishahara na **shilingi**

**159,928,750/=** kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kwa upande wa mapato program hii ilipanga kukusanya shilingi **40,000,000/-** hadi kufikia machi 2023 wizara ya afya Pemba ilikusanya **22,499,000/-** sawa na asilimia **56.2** ya makadirio**.**

110. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 Wizara ya Afya Pemba imepata mafanikio makubwa katika kuimarisha utoaji wa huduma za afya yakiwemo; kufanya tafiti mbalimbali zikiwemo za maradhi ya kichocho, minyoo ya tumbo, afya ya mama na mtoto na korona (COVID 19) kwa lengo la kuimarisha afya za wananchi. Kupitia tafiti hizo ripoti kamili zinapatikana katika Maabara ya Afya ya Jamii (PHL) iliyopo Pemba. Katika kuimarisha utoaji wa huduma kwa Hospitali na vituo vya afya Wizara imefanikiwa kuanzisha huduma za upasuaji, figo, moyo, shinikizo la damu, kisukari na huduma za mama na mtoto.

111. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha nguvu kazi ya Sekta ya Afya, wafanyakazi **39** wameruhusiwa kwenda masomoni wakiwemo madaktari, wauguzi, mafundi sanifu na kada nyengine zisizo cha afya. Jumla ya wafanyakazi **wanne** wamerudi kutoka masomoni. Aidha malipo ya likizo la kawaida kwa wafanyakazi 4**2** yalifanyika.

112. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyengine jumla ya wafanyakazi **261** wameajiriwa hadi kufikia Machi 2023. Miongoni mwao ni Daktari **16**, Afisa Tabibu **30**, Afisa Tabibu Meno **13**, Mfamasia 33, Fundi Sanifu Madawa **10**, Afisa maabara **10**, Msaidizi Daktari **19**,

Afisa mazingira **13**, Wauguzi **113**, Mzoeza Viungo **wawili** na Afisa **ushauri** nasaha **wanne**. Aidha wafanyakazi **34** wamestaafu kwa mujibu wa taratibu za kiutumishi. Aidha, wafanyakazi **saba** wamefariki dunia, Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema Peponi, Amiin.

**PROGRAMU YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA (HO2)**

**113. Mheshimiwa Spika,** Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa mwaka wa Fedha 2022/2023, ilipangiwa kutumia shilingi **34,186,349,000/=** ikiwa shilingi **14,694,200,000/=** kwa mishahara, Shilingi **5,969,930,000/=** kwa matumizi ya uendeshaji wa hospitali, na na shilingi **13,522,219,000/=** kwa Miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi 2023 jumla ya shilingi **19,507,633,243/=** ziliingizwa kwa matumizi mbali mbali ambapo shilingi **17,369,013,343/=** ni kwa mishahara. Ongezeko hili ni kutokana na mbadiliko ya mishahara yalioanza Julai 2022 na shilingi **2,138,619,900/=** kwa uendeshaji. **Kiambatisho nambari 1** kinafafanua.

**114. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeingiziwa fedha maalum shilingi **2,130,000,000/=** kwa matumizi ya dawa na vifaa tiba na shilingi **597,405,350/=** kwa matumizi ya tiba hewa ambalo ni hamisho la fungu (virement) kutoka Wizara ya Afya (H01). Aidha, kwa upande wa Miradi ya Maendeleo hakukuwa na fedha iliyopatikana kwa fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kwa upande wa Washirika wa Maendeleo, Jumla ya shilingi **681,310,000/=** sawa na asilimia **9.0** zimeingizwa moja kwa moja kwa Kitengo cha Utekelezaji wa Mradi (PIU) kama mishahara ya watendaji wa PIU.

115. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa makusanyo, Hospitali ya Mnazi Mmoja ilikadiriwa kukusanya shilingi **1,000,000,000/=** kupitia vyanzo vya malipo ya Huduma za Afya, Huduma za Haraka (Fast Track) huduma za Bima na malipo ya wanafunzi wa kigeni. Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 jumla ya shilingi **707, 106,743.68/=** sawa na asilimia **96** zilikusanywa**. Kiambatisho nambari 2** kinafafanua.

**PROGRAMU NDOGO YA UCHUNGUZI NA MATIBABU**

116. **Mheshimiwa Spika,** Huduma za uchunguzi ni muhimu katika kutoa matibabu sahihi kwa mgonjwa. Katika kipindi hichi cha utekelezaji, jumla ya vipimo vya maabara **106,238** vilifanyika na vipimo **27,499** kwa njia ya picha (Ultrasound ni **12,110**; Xray **10,823**, MRI **1,145**; na CT scan **3,421**) vilifanyika. Kwa upande wa uchunguzi wa maiti zinazohusiana na kesi za Jinai, matukio ya mashambulio ya kuumiza mwili na matukio yote ya kesi za udhalilishaji katika kituo cha mkono kwa mkono zimefanyiwa kazi. Jumla ya maiti 174 zinazohusiana na kesi za Jinai, ajali za barabarani, moto na kuzama baharini zimefanyiwa uchunguzi, kesi za mashambulio ya kuumiza mwili **1,020** na kesi za udhalilishaji **840** zimefanyiwa uchunguzi.

117. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha huduma za wagonjwa, matibabu mbali mbali yameendelea kutolewa ikiwemo huduma za dharura, kilinik za maradhi maalum kama vile Saratani, Moyo, Ngozi, Mifupa n.k. Hadi kufikia Machi 2023 jumla ya wagonjwa

wa nje **106,378** walitibiwa kati ya hao wagonjwa **19,425** walilazwa, Pia wajawazito **17,542** walipokelewa kwa kujifunguwa ambapo wajawazito **12,579** ndio walijifunguwa kati yao wajawazito **2,727** walijifungua kwa njia ya Upasuaji.

**118. Mheshimiwa Spika,** Huduma za kusafisha damu kwa wagonjwa wenye matatizo ya Figo (Dialysis) kwa wagonjwa wenye matatizo ya figo ziliendelea kutolewa bila ya malipo kwa wagonjwa **350** wakiwemo wagonjwa wapya **46**. Aidha mahudhurio ya wagonjwa **1,526** yalifanyika katika kliniki ya saratani kwa ajili ya kupatiwa huduma; saratani ya tenzi dume wagonjwa **66** wapya, Saratani ya matiti wagonjwa **36** wapya na saratani ya mlango wa kizazi kwa wagonjwa **26** wapya. Katika hatua nyengine mahudhurio ya wagonjwa **5,457** wamepata matibabu katika kliniki maalumu ya maradhi ya moyo ambapo wagonjwa **521** ni wapya, na wagonjwa **4,936** wa marejeo.

**119. Mheshimiwa Spika,** Jumla ya kambi 30 zilifanyika na wagonjwa **3,829** walichunguzwa na kupatiwa matibabu. Kati ya hao wagonjwa **717** walifanyiwa upasuaji. Kwa wagonjwa wote hawa zimeokolewa fedha nyingi za serikali. Aidha, dawa na vifaa tiba muhimu ziliendelea kupatikana kama vile dawa za saratani, Kisukari, shinikizo la damu pamoja na ununuzi wa mahitaji ya huduma za dialysis, vyuma kwa huduma za upasuaji wa mifupa pamoja na vitendanishi.

**PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA.**

**120. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha utoaji wa huduma jumla ya wafanyakazi 32 wakiwemo madaktari bingwa, wauguzi na wafanyakazi wasio wa kada ya afya waliomaliza masomo ya muda mrefu wamerudi kazini. Aidha, wafanyakazi mbali mbali wamepatiwa mafunzo ya kuengeza ujuzi yakiwemo mafunzo ya ultrasound, Helping Babies to Breath (HBB), mafunzo ya huduma ya dharura na matumizi sahihi ya Oxygen, mafunzo ya Ebola, mafunzo ya kutumia dawa za kusafishia, udhibiti wa taka za hospitali, usafi wa mikono, usalama wa chakula na usafi wa mazingira maeneo ya kazi, mafunzo ya kuwasaidia watoto wanaozaliwa utumbo nje.

**121. Mheshimiwa Spika,** Ukarabati wa majengo ya Hospitali ya wagonjwa wa akili umekamilika kwa awamu ya kwanza na kuanza kutumika kwa utoaji wa huduma. Vilevile mfumo mpya wa hewa ya Oxygen katika vyumba vya upasuaji vya Idara ya Pua, Masikio na Koo (ENT) umefungwa.

**122. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha mashirikiano na taasisi za kimataifa zikiwemo Hospitali ya Chuo Kikuu cha Haukeland ya Norway, Hospitali ya Chuo Kikuu cha Alexandria kupitia mashirikiano na "Nile Hope Foundation" ya Misri. Mashirikiano hayo yanajumuisha mafunzo, kubadilishana wataalamu na kufanya kambi za matibabu, upatikanaji wa vifaa tiba na kuimarisha miundombinu ya Hospitali. Sambamba na hilo, Mradi

shirikishi wa kuimarisha huduma za macho (CBM), mradi wa kubadilishana wataalamu wa Afya (NOREC EXCHANGE PROGRAM) na mradi wa Ukarabati na utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja (BADEA) iliendelea kutekelezwa.

**UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO**

**123. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2022/23, Hospitali ya MnaziMmoja umepangiwa kutekeleza mradi wa kupandisha hadhi hospitali ya MnaziMmoja ambapo imefanikiwa ununuzi wa vifaa tiba mbali mbali na mashine za hospitali vikiwemo vifaa vya huduma za urology, machine za kitengo cha masikio pua na koo pamoja na tanuri la kuchomea taka kwa hospitali ya wagonjwa wa akili.

**124. Mheshimiwa Spika,** Wizara imepokea mkopo nafuu kupitia Shirika la fedha Duniani (IMF) wenye lengo la kusaidia nchi ambazo zimeathirika na ugonjwa wa UVIKO 19, ili kukabiliana na hali ya kiuchumi na kijamii kwa sekta ambazo zimeathiriwa na ugonjwa huo. Kwa kutumia fedha hizo, Wizara imefanikiwa kukamilisha ujenzi wa Hospitali **10** za Wilaya na **moja** ya Mkoa. Hospitali hizo ni Mwera Pongwe (Wilaya ya Kati), Kitogani (Wilaya ya Kusini), Chumbuni (Wilaya ya Mjini), Magogoni (Wilaya ya Magharibi B), Mbuzini (Wilaya ya Magharibi A), Pangatupu (Wilaya ya Kaskazini B) na Kivunge (Wilaya ya Kaskazini A) kwa upande wa Kisiwa cha Unguja. Kwa upande wa Kisiwa cha Pemba ni Kinyasini (Wilaya ya Wete), Micheweni (Wilaya ya Micheweni) na Vitongoji (Wilaya ya Chake Chake). Pia ujenzi wa hospitali ya

Mkoa katika eneo la Lumumba (Mkoa wa Mjini Magharibi) umekamilika. Kwa upande wa vifaa tiba vimeanza kuingia nchini kwa ajili ya hospitali hizo. Aidha gari 12 za kubebea wagonjwa (ambulance) zimenunuliwa kwa ajili ya utekelezaji wa mfumo rufaa katika ngazi ya Wilaya na Mkoa. Katika hatua ya kuimarisha huduma za dharura, Wizara imekamilisha ujenzi wa jengo la huduma za dharura katika hospitali ya Makunduchi na kuanza kutoa huduma. Sambamba na hilo wafanyakazi wa hospitali hizo mpya wameajiriwa na tayari wapo kazini.

**CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

**125. Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mafanikio mengi yaliyopatikana katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara pia imepitia changamoto nyingi kama ifuatavyo: -

i. Uhaba wa wataalamu wakiwemo madaktari, wataalamu wa ganzi na usingizi, biomedical wahandisi, wauguzi;

ii. Uhaba wa vitendeakazi vya TEHAMA hali inayopelekea kusuasua kwa utekelezaji wa mpango mkakati wa digitali za afya Zanzibar;

iii. Uhaba wa fedha za kufundishia wataalamu

iv. Ukosefu wa vifaa vya kutendea kazi kwa maeneo ya utoaji wa huduma za afya

v. Uchakavu wa miundombinu ikiwemo majengo, machine na vifaa tiba.

vi. Ukosefu wa majengo kwa ajili ya afisi yakiwemo afya za Wilaya na Afisi za Mabaraza ya wataalamu.

## MWELEKEO WA BAJETI NA VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA 2023/2024

## SHUGHULI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA NA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA 2023/2024

**126. Mheshimiwa Spika,** Wizara itaendeleza kukamilisha kazi zinazoendelea katika mwaka 2022/2023 na kutekeleza shughuli zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Aidha, Wizara imejikita zaidi kuongeza mashirikiano na washirika wa Sekta ya Afya, kama ilivyoainishwa katika mkutano wa 13 wa mapitio ya sekta ya afya "**Ubora na Usawa kupitia mageuzi ya kifedha na mashirikiano ya Sekta ya Umma na Binafsi kwa Mfumo thabit wa Afya**" katika kutekeleza kauli mbiu hiyo, Wizara itaelekeza nguvu zake katika kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

i. Kuimarisha miundombinu ya afya katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya.

ii. Kuhakiksha upatikanaji wa Dawa na Vifaa Tiba

iii. Kuimarisha mifumo ya taarifa za afya

iv. Kuimarisha ubora na kuongeza idadi ya rasilimali watu

v. Kutekeleza mpango mkakati wa miaka mitano wa kugharamia huduma za afya.

vi. Kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto wachanga

vii. Kuimarisha uwezo na utayari wa kukabiliana na majanga ya mripuko na matukio mengine ya kiafya.

viii. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za mfuko wa afya Zanzibar kwa wanachama.

ix. Kuendeleza mapambano ya maradhi ya kuambukiza na yasioambukiza

x. Kuimarisha huduma za afya ya msingi.

xi. Kuendeleza kufanya tafiti mbalimbali za kiafya kwa lengo la kujua changamoto zilizopo na namna ya kuzitatua

xii. Kufanya mafunzo kwa wafanyakazi kwa lengo la kuboresha utoaji wa Huduma bora kwa wananchi

**MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024**

127. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kwamba vipaumbele vilivyowekwa vinafikiwa, Wizara kwenye mwaka wa fedha 2023/ 2024 itatekeleza malengo yake kupitia programu husika kama ifuatavyo: -

**PROGRAMU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA**

128. **Mheshimiwa Spika**, katika kufanikisha utekelezaji wa malengo ya Wizara yaliyopangwa kutekelezwa kupitia programu ya Kinga na Elimu ya Afya, Wizara imetenga jumla ya **Shilingi 36,898,364,000/=** ambazo ni sawa na **asilimia 19.4** ya bajeti ya Wizara kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuendelea kudhibiti maambukizi ya VVU kwa kutoa huduma za ushauri nasaha, upimaji na matibabu;

ii. Kuendelea kutoa huduma za tiba kwa wagonjwa wa Kifua Kikuu, Ukoma na Homa ya Ini;

iii. Kuimarisha huduma za afya ya uzazi wa mama na mtoto;

iv. Kuendelea na utekelezaji wa mikakati ya kumaliza Malaria Zanzibar;

v. Kuimarisha huduma za Afya ya Bandari;

vi. Kuendelea kutoa huduma za uchunguzi na tiba kwa maradhi ya macho katika skuli, vituo vya afya na hospitali;

vii. Kuendelea na mikakati ya kupambana na Maradhi yanayoambukiza na yasiyoambukiza;

viii. Kuendelea na mkakati wa kubadilisha tabia hatarishi zinazochangia kuenea kwa maradhi yasiopewa kipaumbele hapa Zanzibar;

ix. Kuimarisha afya ya jamii na mazingira;

x. Kuendelea kufanya tafiti mbali mbali zitakazotoa ili kuimarisha huduma za afya katika kupambana na maradhi;

xi. Kuimarisha program za uhamasishaji na kutoa elimu ya afya katika ngazi zote.

xii. Kuendelea kuimarisha kupambana na maradhi ya mripuko na majanga ya kiafya.

## PROGRAMU YA TIBA

**129. Mheshimiwa Spika**, ili kuhakikisha kwamba huduma za uchunguzi na matibabu zinaimarika zaidi, Wizara imetenga **Shilingi 117,047,946,000/=** sawa na **asilimia 61.8** kati ya hizo shilingi **112,466,846,000/=** kwa ajili ya program ya matibabu na shilingi **4,581,100,000/=** kwa ajili ya program ya Uchunguzi. Shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa: -

i. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za matibabu katika hospitali za wilaya na mkoa

ii. Kutekeleza mfumo wa rufaa kwa wagonjwa katika ngazi zote za utoaji wa huduma.

iii. Kuimarisha kambi za matibabu na mashirikiano ya huduma za afya kimataifa.

iv. Kuongeza ukusanyaji wa damu ili kukidhi mahitaji yaliyopo.

v. Kuhakikisha upatikanaji wa Dawa, Vifaa tiba na reagents

vi. Kuimarisha huduma za uchunguzi (maabara na rediolojia)

vii. Kuimarisha miundombinu ya afya katika ngazi zote za utoaji wa huduma za Afya.

viii. Kuimarisha usimamizi katika uhifadhi na utumiaji wa dawa na vifaa vya utibabu katika hospitali na vituo vya afya.

ix. Kuimarisha utoaji wa huduma kwa wahanga wa udhalilishaji.

x. Kuimarisha uratibu wa huduma za uuguzi na ukunga.

**PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA AFYA**

**130. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara imetenga **Shilingi 35,433,127,000/-** sawa na **asilimia 18.7** kwa ajili ya kutekeleza shughuli kuu zilizopangwa katika programu hii, ambapo **shilingi 2,665,598,000/=** zitatumika kwa shughuli za uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti **shilingi 9,878,103,000/=** kwa ajili ya Utumishi na Uendeshaji, shilingi **481,500,000/-** kwa ya Taasisi ya Utafiti. Aidha Wizara imetenga shilingi **22,407,926,000/-** kwa ajili ya Uratibu na utekelezaji wa shughuli za Afya Pemba. Shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: -

i. Kupeleka masomoni Madaktari na wafanyakazi wa kada nyengine za afya;

ii. Kuendelea kufanya tafiti mbali mbali zikiwemo tafiti za mimea inayotumika kwa Tiba asili;

iii. Kufanya vikao vya pamoja na washirika mbali mbali wa masuala ya Afya ili kutatua changamoto kwa nguvu ya pamoja;

iv. Kufanya ufuatiliaji wa sera na miongozo ya utoaji huduma za afya.

v. Kufanya ufuatiliaji na tathmini katika ngazi zote za utoaji wa huduma.

vi. Kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa takwimu za afya

## PROGRAMU YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA

131. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa 2023/2024, Serikali imetenga shilingi **49,772,000,000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ambazo ni: **-**

i. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za uchunguzi kwa wagonjwa kupitia uwakala (Outsourcing) pamoja na upatikanaji wa huduma za matibabu ya rufaa.

ii. Kuendelea kutoa huduma za kibingwa ikiwemo usafishaji damu kwa wagonjwa wa figo, uchunguzi wa saratani (biopsy), matibabu ya satarani (Chemotherapy), huduma za ubongo na uti wa mgongo n.k

iii. Kupunguza idadi ya wagonjwa wanaopewa rufaa nje ya nchi kwa uimarishaji wa kambi maalum za matibabu na kuwajengea uwezo wataalamu wetu.

iv. Kushajihisha zaidi kufanya tafiti za afya.

v. Kuongeza idadi ya wataalam bingwa kwa kusomesha wataalamu wa fani mbali mbali.

vi. Kuimarisha mfumo wa kielektroniki wa kuhifadhi taarifa za wagonjwa Electronic Medical Record (EMR).

vii. Kuimarisha miundo mbinu ya Hospitali kwa ukarabati mkubwa na upanuzi wa hospitali ambao utaambatana na manunuzi ya mashine za kisasa na samani za hospitali kupitia mradi wa BADEA, Saudi na Kuwait fund ambapo mshauri elekezi ameshapatikana.

viii. Kuendelea na mradi wa CBM kwa lengo la uimarishaji wa huduma shirikishi za macho.

## SHUKRANI

132. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha uliopita, Wizara imeweza kupata mafanikio makubwa, ikiwemo kuimarika kwa miundombinu, vifaa vya utibabu, kuimarika kwa upatikanaji wa dawa na kuongezeka kwa wataalamu wa fani mbali mbali za afya pamoja na Teknologia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa utoaji wa huduma za afya**.** Mafanikio yote haya yanatokana na juhudi za Serikali na washirika mbali mbali wa sekta ya afya, ikiwemo mchango mkubwa kutoka katika jamii, washirika wa maendeleo, pamoja na Taasisi binafsi. Wizara inawashukuru wale wote waliochangia mafanikio haya kwa njia moja au nyengine katika kufanikisha sera ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kutoa huduma za afya bure. Aidha, kwa dhati kabisa nawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Afya kwa kujituma kwa moyo katika kuwahudumia wananchi.

133. **Mheshimiwa Spika,** sasa naomba uniruhusu kuyashukuru Mashirika mbali mbali ya Maendeleo yakiwemo Shirika la Afya la Ulimwenguni -WHO, UNICEF, UNFPA, Danida, Haukeland University Hospital ya Norway, SAVE THE CHILDREN, Engender Health, D-Tree International, World Diabetic Foundation, World Bank, CDC, AMREF, Sight Saver, HIPZ, USAID Afya yangu, Mfuko wa kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria (GFATM), Measure Evaluation, Mfuko wa Rais wa Marekani (PMI), THPS,

DFID, JHPU, IHI, WATER AID, WAJAMAMA, JICA, STBF, PEPFAR, ZOP, UNDP, EAC, Benjamin Mkapa Foundation, Tonny Blair Institute, Zanzibar Maisha Bora Foundation na Zanzibar Milele Foundation. Aidha napenda kuzishukuru nchi rafiki kwa mashirikiano yao zikiwemo, Jamhuri ya watu wa China, Serikali ya Cuba, Serikali ya Denmark, Uholanzi, Spain, Canada, Israel, Norway, Ujerumani, Korea, Uturuki, India, Kuwait, Marekani, Italy, Saudi Arabia, Oman, UAE, Uingereza. Aidha, tunatoa shukrani kwa Wizara zote za SMZ pamoja na sekta mbali mbali za Serikali na Binafsi. Sekta hizi zimesaidia sana kwa namna moja ama nyengine katika kuhakikisha jamii inapata huduma za afya kwa wote.

## HITIMISHO

## MAOMBI YA FEDHA KWA UTEKELEZAJI WA KAZI ZILIZOPANGWA KWA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

134. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Afya (Fungu H01) inakadiriwa kutumia kiasi cha **Shilingi 189,379,436,000/=** Kati ya hizo **Shilingi 60,013,800,000/-** kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 58,627,086,000/=** kwa matumizi mengineyo na **Shilingi 5,062,600,000/=** ni ruzuku kwa taasisi zilizo chini ya Wizara **(Kiambatisho Namba 6)** kinafafanua.

135. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa kazi za maendeleo, Wizara imepangiwa kutumia **Shilingi 65,675,951,000/=** kati ya hizo, **Shilingi 53,050,000,000/=** kutoka serikalini na **Shilingi 12,625,951,000/=** ni kutoka kwa washirika wa maendeleo. Aidha, hospitali ya Mnazi Mmoja imepangiwa kutumia **Shilingi 49,772,000,000/=**; kati ya hizo **Shilingi 24,372,400,000/=** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 14,274,400,000** kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji wa hospitali na shilingi **11,125,200,000/=** kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kati ya hizo shilingi **1,125,200,000/-** kutoka serikalini na shilingi **10,000,000,000/-** kutoka kwa washirika wa maendeleo**.**

136. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mapato, wizara (Fungu H01) imepangiwa kukusanya **shilingi 5,751,881,000/=** kwa ajili ya kuchangia katika mfuko mkuu wa Serikali. Hospitali ya Mnazi

Mmoja (Fungu H02) imepangiwa kukusanya shilingi **1,348,585,000/=** kutoka katika vyanzo vyake mbali mbali vya mapato.

137. **Mheshimiwa Spika,** sasa naomba Wajumbe wa kamati yako waijadili hotuba hii na hatimae waridhie matumizi ya Shilingi **189,379,436,000/=** kwa Wizara ya Afya (Fungu H01) na **Shilingi 49,772,000,000/=** kwa matumizi ya Hospitali ya Mnazi Mmoja (Fungu H02). Aidha, waridhie makusanyo ya **shilingi 5,751,881,000/=** kwa Wizara ya Afya na shilingi **1,348,585,000/=** kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa ajili ya kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

138. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**NASSOR AHMED MAZRUI (MBM)**

**WAZIRI WA AFYA,**

**ZANZIBAR.**

**_Kiambatisho Namba 1:_** Muhtasari wa Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Afya (Julai, 2022- Machi, 2023)

| Programu Kuu/Programu Ndogo | Fungu | Makisio ya Mwaka 2022/2023 | Makisio ya Fedha Julai,2022 hadi Machi 2023 | Fedha zilizopatikana Julai,2022 hadi Machi 2023 | Asilimia ya Fedha iliyopatikana Julai,2022 hadi Machi 2023 | Asilimia ya Fedha iliyopatikana 2022/2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Programu ya Kinga na Elimu ya Afya(PHO301)** | | | | | | |
| **PH01:** Kinga na Elimu ya Afya | Mishahara | 13,095,316,000 | 9,821,487,000 | 15,307,959,675 | 156 | 116.9 |
| | Matumizi mengineo(OC) | 7,582,282,938 | 5,686,712,204 | 460,517,898 | 8 | 6.1 |
| | Fedha za Maendeleo(SMZ) | 2,125,200,000 | 1,593,900,000 | - | - | 0.0 |
| | Fedha za Maendeleo(Mhisani) | 10,082,700,000 | 7,562,025,000 | 8,097,315,881 | 107 | 80.3 |
| | Pemba | 1,524,614,062 | 1,143,460,547 | 345,410,231 | 30 | 22.7 |
| | **JUMLA** | **34,410,113,000** | **25,807,584,750** | **24,211,203,685** | **94** | **70.4** |
| **Programu ya Tiba (PHO302)** | | | | | | |
| **PH201:** Programu ndogo ya huduma za matibabu | Mishahara | 5,246,809,000 | 3,935,106,750 | 7,479,311,762 | 190 | 142.5 |
| | Matumizi mengineo(OC) | 36,035,104,222 | 27,026,328,167 | 12,805,572,425 | 47 | 35.5 |
| | Pemba | 1,691,445,778 | 1,268,584,334 | 428,810,122 | 34 | 25.4 |
| | **JUMLA** | **42,973,359,000** | **32,230,019,250** | **20,713,694,309** | **64** | **48.2** |
| **Programu ya Tiba (PHO302)** | | | | | | |
| **PH202:** Programu ndogo ya huduma za Uchunguzi | Ruzuku Mishahara | 1,352,819,181 | 1,014,614,386 | 1,866,806,048 | 184 | 138.0 |
| | Ruzuku Matumizi mengineo(OC) | 1,337,803,110 | 1,003,352,333 | 686,638,770 | 68 | 51.3 |
| | Fedha za Maendeleo(SMZ) | 18,569,567,000 | 13,927,175,250 | 1,893,738,719 | 14 | 10.2 |
| | Fedha za Maendeleo(Mhisani) | 25,448,000,000 | 19,086,000,000 | - | - | 0.0 |
| | Ruzuku Pemba (OC) | 433,333,330 | 324,999,998 | 135,202,200 | 42 | 31.2 |
| | Ruzuku Pemba (Mshahara) | 375,744,379 | 281,808,284 | 412,075,745 | 146 | 109.7 |
| | **JUMLA YA MSHAHARA** | **47,517,267,000** | **35,637,950,250** | **4,994,461,482** | **14** | **10.5** |
| **Programu ya Uratibu wa Wizara ya Afya (PH0103)** | | | | | | |
| **PH010301:** Programu ndogo ya Uongozi na Utawala | Mishahara | 3,708,640,200 | 2,781,480,150 | 1,973,165,921 | 71 | 53.2 |
| | Matumizi mengineo(OC) | 5,334,370,800 | 4,000,778,100 | 3,286,407,099 | 82 | 61.6 |
| | **JUMLA YA MSHAHARA** | **9,043,011,000** | **6,782,258,250** | **5,259,573,020** | **78** | **58.2** |
| **Programu ya Uratibu wa Wizara ya Afya (PHO303)** | | | | | | |
| **PH0302:** Programu ndogo ya Mipango,Sera na Utafiti | Mishahara | 817,605,800 | 613,204,350 | 467,512,290 | 76 | 57.2 |
| | Matumizi mengineo(OC) | 1,108,921,200 | 831,690,900 | 83,809,727 | 10 | 7.6 |
| | **JUMLA** | **1,926,527,000** | **1,444,895,250** | **551,322,017** | **38** | **28.6** |

• • •

## ***Kiambatisho Namba 1:*** Muhtasari wa Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Afya (Julai, 2022- Machi, 2023)

| Programu Kuu/Programu Ndogo | Fungu | Makisio ya Mwaka 2022/2023 | Makisio ya Fedha Julai,2022 hadi Machi 2023 | Fedha zilizopatikana Julai,2022 hadi Machi 2023 | Asilimia ya Fedha iliyopatikana Julai,2022 hadi Machi 2023 | Asilimia ya Fedha iliyopatikana 2022/2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Programu ya Uratibu wa Wizara ya Afya (PHO303)** | | | | | | |
| **PH0302:** Programu ndogo ya Uratibu wa shughuli za Afya Pemba | Mishahara | 12,651,527,000 | 9,488,645,250 | 15,295,470,272 | 161 | 120.9 |
| | Matumizi mengineo(OC) | 363,305,000 | 272,478,750 | 159,928,750 | 59 | 44.0 |
| | **JUMLA** | **13,014,832,000** | **9,761,124,000** | **15,455,399,022** | **158** | **118.8** |
| **Programu ya Uratibu wa Wizara ya Afya (PHO303)** | | | | | | |
| **PH0302:** Programu ndogo ya tafiti za Afya | Matumizi mengineo(OC) | 642,000,000 | 481,500,000 | 154,650,000 | 32 | 24.1 |
| | Fedha za Maendeleo(SMZ) | 4,500,000,000 | 3,375,000,000 | | - | 0.0 |
| | **JUMLA** | **5,142,000,000** | **3,856,500,000** | **154,650,000** | **4** | **3.0** |
| **JUMLA KUU(H01)** | | **154,027,109,000** | **115,520,331,750** | **71,340,303,535** | **62** | **46.3** |
| **Hospital ya Mnazi Mmoja (HO2)** | | | | | | |
| **PH0201:** Programu ndogo ya huduma za Uchunguzi na matibabu | Matumizi mengineo(OC) | 3,340,529,000 | 2,505,396,750 | 267,798,216 | | 8.0 |
| | **JUMLA** | **3,340,529,000** | **2,505,396,750** | **267,798,216** | | **8.0** |
| **Programu ya Uratibu wa Wizara ya Afya (PHO303)** | | | | | | |
| **PH0202:** Programu ndogo ya Uongozi na Utawala | Mishahara | 14,694,200,000 | 11,020,650,000 | 17,369,013,343 | 158 | 118.2 |
| | Matumizi mengineo(OC) | 4,829,401,000 | 3,622,050,750 | 2,138,619,900 | 59 | 44.3 |
| | Fedha za Maendeleo(SMZ) | 5,553,000,000 | 4,164,750,000 | - | - | 0.0 |
| | Fedha za Maendeleo(Mhisani) | 7,969,219,000 | 5,976,914,250 | 681,310,000 | 11 | 8.5 |
| | **JUMLA** | **33,045,820,000** | **24,784,365,000** | **20,188,943,243** | **81** | **61.1** |
| **JUMLA KUU (H02)** | | **36,386,349,000** | **27,289,761,750** | **20,456,741,459** | **75** | **56.2** |
| **JUMLA YA WIZARA** | | **190,413,458,000** | **142,810,093,500** | **91,797,044,994** | **64** | **48.2** |

## *Kiambatisho Namba 2:* Muhtasari wa Makusanyo ya Wizara ya Afya (Julai, 2022- Machi, 2023)

| Kifungu | KASMA | MAELEZO | Makadirio ya Makusanyo kwa Mwaka 2022/23 | Makadirio ya Makusanyo kwa Julai 2022 hadi Machi 2023 | Fedha zilizokusanywa Julai 2022 hadi Machi 2023 | Makadirio ya Makusanyo kwa Aprili 2023 hadi Juni 2023 | Asilimia ya Makusanyo Julai 2022 hadi Machi 2023 | Asilimia ya Makusanyo kwa Mwaka 2022/23 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Programa ya Kinga na Elimu ya Afya (PH0101)** | | | | | | | |
| H0301 | 1422035 | Shahada ya Maradhi ya kuambukiza | 118,000,000 | 88,500,000 | 59,288,400.00 | 19,762,800.00 | 67 | 50 |
| | 1422050 | Ada ya uchunguzi wa vyombo vya usafiri wa abiria | 64,000,000 | 48,000,000 | 77,097,961.99 | 25,699,320.66 | 161 | 120 |
| | 1422051 | Uchunguzi wa afya ya wafanyakazi | 96,000,000 | 72,000,000 | 83,627,701.00 | 27,875,900.33 | 116 | 87 |
| | | Ukodishwajiwa maeneo ya kibiashara -RCH | 15,000,000 | 11,250,000 | 20,374,594.24 | 6,791,531.41 | 181 | 136 |
| | | Ukodishwajiwa maeneo ya kibiashara -MALARIA | 8,000,000 | 6,000,000 | 3,100,000.00 | 1,033,333.33 | 52 | 39 |
| | 1422078 | Ukodishwaji wa maeneo ya kibiashara-UKIMWI | 10,000,000 | 7,500,000 | 100,000.00 | 33,333.33 | 1 | 1 |
| | | UVIKO 19 | 24,191,000,000 | 18,143,250,000 | 1,699,751,245.24 | 566,583,748.41 | 9 | 7 |
| | | **Jumla Ndogo** | **24,502,000,000** | **18,376,500,000** | **1,943,339,902.47** | **647,779,967.49** | **11** | **8** |
| | | **Program ya Tiba (PH0102)** | | | | | | |
| H0302 | 1422095 | Ada ya Usajili wa Tiba Asili | 60,000,000 | 45,000,000 | 32,527,400.00 | 10,842,466.67 | 72 | 54 |
| | 1422118 | Usajili na Leseni Wauguzi | 57,000,000 | 42,750,000 | 53,920,454.01 | 17,973,484.67 | 126 | 95 |
| | 1422118 | Usajili na Leseni Madaktari | 70,000,000 | 52,500,000 | 98,021,049.63 | 32,673,683.21 | 187 | 140 |
| | 1422118 | Usajili na Leseni wataalamu wa Afya ya Mazingira | 15,000,000 | 11,250,000 | 17,315,880.00 | 5,771,960.00 | 154 | 115 |
| | 1422118 | Usajili na Leseni kwa Huduma Hospitali Binafsi | 100,000,000 | 75,000,000 | 65,409,979.00 | 21,803,326.33 | 87 | 65 |
| | 1422118 | Usajili na Leseni Waaalamu wa Maabara | 60,000,000 | 45,000,000 | 12,517,036.00 | 4,172,345.33 | 28 | 21 |
| | | **Jumla Ndogo** | **362,000,000** | **271,500,000** | **279,711,798.64** | **93,237,266.21** | **103** | **77** |
| | **Program ya Uratibu wa Sera za Afya na Utawala (PH0103)** | | | | | | | |
| H0305 | 1422051 | Huduma za Uchunguzi wa Afya Pemba | 20,000,000 | 15,000,000 | 21,516,319.99 | 7,172,106.66 | 143 | 108 |
| | 1422094 | Tasisi ya Utafiti wa Afya | 45,000,000 | 33,750,000 | 57,058,430.00 | 19,019,476.67 | 169 | 127 |
| | 1422084 | Nyaraka za Zabuni | 71,000,000 | 53,250,000 | - | - | - | - |
| | | **Jumla Ndogo** | **136,000,000** | **102,000,000** | **78,574,749.99** | **26,191,583.33** | **77** | **58** |
| | **JUMLA KUU KWA FUNGU H01** | | **25,000,000,000** | **18,750,000,000** | **2,301,626,451.1** | **767,208,817.03** | **12** | **9** |
| | **Makusanyo Mnazi Mmoja Hospital(PH02)** | | | | | | | |
| H02 | 1422051 | Huduma za Haraka(First Track) | 1,000,000,000 | 750,000,000 | 707,106,743.00 | 235,702,247.67 | 94 | 71 |
| | **JUMLA KUU KWA FUNGU H02** | | **1,000,000,000** | **750,000,000** | **707,106,743.00** | **235,702,247.67** | **94** | **71** |

***Kiambatisho Namba 3a:*** Kiwango cha Chanjo Kiwilaya Mwaka 2022

| Wilaya | Chanjo ya Kukinga Ugonjwa wa Kifua Kikuu (BCG) | (Chanjo ya Kukinga Ugonjwa wa Kifaduro, Pepo Punda, Degedege, Uti wa Mgongo na Homa ya Ini (Penta 3) | Chanjo ya Kukiknga Ugonjwa wa Pepo Punda (TT2+) kwa Vijana wa Kike Wenye Umri wa Kuzaa | Chanjo ya Kukiknga Ugonjwa wa Pepo Punda (TT2+) kwa kwa mama Wajawazito | Chanjo ya Kukinga Ugonjwa wa Surua (Measles) | Walio-kamilisha Chanjo | Chanjo ya kujikinga na Kansa ya shingo ya kizazi (HPV vaccine) kwa vijana wa Kike wa Miaka 9-14 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Chakechake | 106.3 | 78.6 | 1.5 | 50.4 | 76.7 | 76.7 | 46.3 |
| Micheweni | 103.9 | 77.9 | 0.48 | 37.5 | 75.7 | 75.5 | 58 |
| Mkoani | 115.5 | 70.4 | 1.5 | 29.4 | 65.8 | 65.8 | 56.5 |
| Wete | 102.1 | 82.4 | 1.5 | 46 | 79.7 | 80.3 | 70.5 |
| Kaskazini A | 139.5 | 93.1 | 4.1 | 38 | 95 | 98.7 | 34.3 |
| Kaskazini B | 83.1 | 80 | 1.6 | 38.7 | 72.4 | 69.3 | 40.1 |
| Kati | 115.2 | 87.6 | 1.6 | 44.8 | 83.4 | 82.5 | 12.8 |
| Kusini | 113 | 105 | 9.5 | 40.7 | 108 | 103.9 | 61.8 |
| Magharibi A | 110.7 | 61.5 | 0.4 | 71.3 | 70.5 | 94.2 | 28.9 |
| Magharibi B | 133.4 | 77.7 | 1.9 | 47.7 | 82.2 | 78.8 | 19.5 |
| Mjini | 129.6 | 70.2 | 2.4 | 28.3 | 73.9 | 72 | 6.4 |

***Kiambatisho Namba 3b:*** Idadi ya Wagonjwa Waliohudhuria Matibabu ya Nje, Waliolazwa na Vifo kwa Mwaka 2022

| Hospital | Wagojwa wa nje | Wagojwa wa ndani | Jumla ya vifo |
|---|---|---|---|
| Abdalla Mzee Regional Hospital | 26,896 | 3,407 | 231 |
| Al-Rahma Hospital | 4,237 | 1,534 | 25 |
| Chakechake District Hospital | 32,219 | 732 | 17 |
| Kivunge District Hospital | 51,656 | 4,230 | 134 |
| KMKM Kibweni Hospital | 119,517 | 1,110 | 45 |
| Makunduchi District Hospital | 29,748 | 1,582 | 23 |
| Micheweni District Hospital | 27,100 | 3,971 | 123 |
| Mnazi Mmoja Hospital | 87,528 | 23,197 | 1,729 |
| Tasakhtaa Global Hospital | 419 | 1,717 | 36 |
| Tawaqal Hospital | 29,738 | 1,819 | 8 |
| Vitongoji Cottage Hospital | 24,395 | 2,141 | 46 |
| Wete District Hospital | 35,669 | 5,623 | 193 |
| Zanzibar Military Hospital (JWTZ-Bububu) | 0 | 611 | 33 |
| **Jumla** | **469,122** | **51,674** | **2,643** |

***Kiambatisho Namba 3c:*** Idadi ya Wajawazito Waliolazwa, Waliojifungua, Watoto Waliozaliwa na Vifo vya Watoto Wachanga kwa Kipindi Julai 2022- Machi 2023

| Aina ya Sehemu | Hospital | Wajawazito waliolazwa | Mama waliojifungua | | Watoto waliozaliwa hai | Vichanga vilivyofariki |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kawaida | Upasuaji | | |
| Pemba | Chakechake District Hospital | 4,428 | 4,114 | 595 | 4,126 | 119 |
| | Abdalla Mzee Regional Hospital | 2,960 | 2,784 | 281 | 2,773 | 100 |
| | Micheweni District Hospital | 3,386 | 2,923 | 233 | 2,920 | 87 |
| | Wete District Hospital | 3,470 | 2,957 | 382 | 2,958 | 71 |
| | Vitongoji Cottage Hospital | 696 | 608 | - | 610 | 7 |
| | PHCU+ | 6,293 | 5,860 | - | 5,936 | 49 |
| | **Jumla Ndogo** | **21,233** | **19,246** | **1,491** | **19,323** | **433** |
| Unguja | Mnazi Mmoja Hospital | 17,860 | 16,449 | 3,725 | 16,350 | 597 |
| | Mwembeladu Hospital | 4,496 | 4,022 | - | 4,030 | 23 |
| | Kivunge District Hospital | 4,621 | 4,425 | 440 | 4,495 | 111 |
| | Makunduchi District Hospital | 1,747 | 1,507 | 222 | 1,511 | 37 |
| | Zanzibar Military Hospital (JWTZ-Bububu) | 310 | 273 | 31 | 267 | 10 |
| | PHCU+ | 3,427 | 3,158 | 9 | 3,178 | 21 |
| | **Jumla Ndogo** | **32,461** | **29,834** | **4,427** | **29,831** | **799** |
| Binafsi | Al-Rahma Hospital | 1,228 | 1,179 | 364 | 1,185 | 9 |
| | Mina Hospital | 164 | 154 | 86 | 163 | 1 |
| | Tasakhtaa Global Hospital | 1,313 | 703 | 37 | 703 | 2 |
| | Tawaqal Hospital | 510 | 512 | 181 | 519 | 6 |
| | KMKM Kibweni Hospital | 782 | 739 | 98 | 749 | 4 |
| | MAYDA Health charitable foundation | 158 | 121 | - | 137 | - |
| | **Jumla Ndogo** | **4,155** | **3,408** | **766** | **3,456** | **22** |
| **JUMLA KUU** | | **57,849** | **52,488** | **6,684** | **52,610** | 1,254 |

***Kiambatisho Namba 3d:*** Idadi ya Wagonjwa Waliohudhuria Kliniki za Matibabu ya Maalumu kwa Mwaka 2022

| Aina ya Kliniki Maalumu | Wanaume | Wanawake | Jumla |
|---|---|---|---|
| Acupuncture | 1,910 | 3,245 | 5,155 |
| Cardiac | 5,535 | 11,053 | 16,588 |
| Dental | 3,315 | 4,273 | 7,588 |
| Diabetic | 17,578 | 24,138 | 41,716 |
| ENT | 13,615 | 19,317 | 32,932 |
| Eye | 29,885 | 38,548 | 68,433 |
| Obsy & Gynae | | 22,592 | 22,592 |
| Neurosurgery | 1,941 | 2,245 | 4,186 |
| Oncology | 1,015 | 1,506 | 2,521 |
| Orthopedic | 1,350 | 1,143 | 2,493 |
| Physio & Rehabilitation | 657 | 818 | 1,475 |
| Psychiatric | 3,391 | 4,462 | 7,853 |
| Skin disease | 3,376 | 7,085 | 10,461 |
| Surgical OPD | 7,255 | 7,024 | 14,279 |
| **Jumla Kuu** | **90,823** | **147,449** | **238,272** |

***Kiambatisho Namba 4:*** Idadi, Aina ya Kambi Zilizofanyika na Idadi ya Wagonjwa Waliopatiwa Matibabu

| Aina ya kambi na Muhusika | Aina ya Huduma | Idadi ya Watu waliofikiwa | Idadi ya Wagojwa Waliopatiwa Matibabu |
|---|---|---|---|
| International Society for Gynaecological Endoscopy- USA | Gynaecological | 3 (Mme-0 na W,ke-3) | 3 Walifanyiwa upasuaji |
| Israel Camp | Othorpedic | 50 (Mme-25 na W,ke-15) | 17 Walifanyiwa upasuaji |
| Chidren Heart Charitable Association-Kuwait | Heart Specialization | 33 (Mme-17 na W,ke-16) | |
| Specticle Care -Norway | Eye Specialist | 1,110 (Mme-304 na W,ke-806) | 148-sunglass, 339-readind glass |
| Pelex Egypt Camp | Obstrectic, Orthopedic, General Surgery Urology | 480 (Wme-230 na Wke-250 | Walifanyiwa upasuaji 298 |

***Kiambatisho Namba 5:*** Aina ya Kada na Wafanyakazi Wapya Walioajiriwa kwa Mwaka 2022-2023

| SN | KADA | IDADI |
|---|---|---|
| 1 | DAKTARI WA BINAADAMU | 122 |
| 2 | DAKTARI WA MENO | 13 |
| 3 | AFISA MAABARA | 15 |
| 4 | AFISA MIONZI | 0 |
| 5 | MFIZIOTHERAPIA | 1 |
| 6 | AFISA AFYA MAZINGIRA | 12 |
| 7 | AFISA USHAURI NASAHA | 18 |
| 8 | MFAMASIA | 30 |
| 9 | MUUGUZI | 50 |
| 10 | AFISA TABIBU | 60 |
| 11 | AFISA TABIBU MENO | 34 |
| 12 | MUUGUZI MSAIDIZI | 214 |
| 13 | AFISA MAABARA MSAIDIZI | 15 |
| 14 | MFIZIOTHERAPIA MSAIDIZI | 20 |
| 15 | AFISA AFYA MAZINGIRAMSAIDIZI | 25 |
| 16 | MFAMASIA MSAIDIZI | 70 |
| 17 | AFISA USHAURI NASAHA MSAIDIZI | 11 |
| **JUMLA** | | **710** |

## *Kiambatisho Namba 6:* Mchanganuo wa Maombi ya fedha kwa mwaka 2023/2024

| Maelezo | Matumizi ya Maendeleo | | | | Matumizi Mengineyo | | Jumla Kuu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mchango wa Serikali | Msaada Washirika wa Maendeleo | Mkopo | Jumla ya fedha za maendeleo | Mshahara | Matumizi ya Kawaida | |
| **Programu ya Kinga na Elimu ya Afya(PHO301)** | | | | | | | |
| Huduma za Kinga na Elimu ya Afya | | | | | 22,225,852,920 | 3,698,371,600 | 25,924,224,520 |
| Mradi shirikishi wa Ukimwi,Homa ya Ini,Kifua Kikuu na Ukoma | 500,000,000 | 1,050,206,229 | | 1,550,206,229 | | | 1,550,206,229 |
| Mradi wa kumaliza Mlaria Zanzibar | 550,000,000 | 977,728,311.00 | | 1,527,728,311 | | | 1,527,728,311 |
| Mradi shirikishi wa Huduma za Afya ya Mama na Mtoto | 1,000,000,000 | 4,808,344,400 | | 5,808,344,400 | | | 5,808,344,400 |
| Pemba | 0 | 0 | 0 | 0 | | 2,087,860,140 | 2,087,860,140 |
| **Jumla Ndogo** | **2,050,000,000** | **6,836,278,940** | | **8,886,278,940** | **22,225,852,920** | **5,786,231,740** | **36,898,363,600** |
| **Programu ya Tiba(PHO102)** | | | | | | | |
| Programu ndogo ya Matibabu(SH0201) | | | | | 9,261,482,600 | 40,782,579,000 | 50,044,061,600 |
| Programu ndogo ya Uchunguzi(SH0202) | | | | | | 3,781,453,080 | 3,781,453,080 |
| Ujenzi wa Kituo cha Afya Kizimkazi | | 4,000,000,000 | | 4,000,000,000 | | | 4,000,000,000 |
| Ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi | 20,000,000,000 | | | 20,000,000,000 | | | 20,000,000,000 |
| Ujenzi na Ukarabati wa vituo vya Afya Msingi | 20,000,000,000 | | | 20,000,000,000 | | | 20,000,000,000 |
| Mradi wa kuimarisha huduma za mama na mtoto | 0 | 0 | 1,789,672,060 | 1,789,672,060 | | | 1,789,672,060 |
| Kuimarisha Mifumo ya Afya | 10,000,000,000 | | | 10,000,000,000 | | | 10,000,000,000 |
| Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Afya | 1,000,000,000 | | | 1,000,000,000 | | | 1,000,000,000 |
| Matibabu Pemba | | | | | | 5,633,112,280 | 5,633,112,280 |
| Uchunguzi Pemba | | | | | | 799,646,920 | 799,645,920 |
| **Jumla Ndogo** | **51,000,000,000** | **4,000,000,000** | **1,789,672,060** | **56,789,672,060** | **9,261,482,600** | **50,996,791,280** | **117,047,944,940** |
| **Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara (PH0103)** | | | | | | | |
| Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji (SH010301) | | | | | 5,388,945,520 | 4,489,157,940 | 9,878,103,460 |
| Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti (SH010302) | | | | | 1,474,092,960 | 1,191,505,040 | 2,665,598,000 |
| Programu ndogo ya Uratibu wa shughuli za Afya Pemba (SH010303) | | | | | 21,663,426,000 | 744,500,000 | 22,407,926,000 |
| Programu ndogo ya Tafiti za Afya (SH010304) | | | | | 0 | 481,500,000 | 481,500,000 |
| **Jumla** | | | | | **28,526,464,480** | **6,906,662,980** | **35,433,127,460** |
| **JUMLA YA FUNGU H01** | **53,050,000,000** | **10,836,278,940** | **1,789,672,060** | **65,675,951,000** | **60,013,800,000** | **63,689,686,000** | **189,379,436,000** |
| **Hospitali ya Mnazi Mmoja (Fungu HO2)** | | | | | | | |
| Programu ndogo ya Uongozi na Utawala (SH0202) | | | | | 24,372,400,000 | 14,274,400,000 | 38,646,800,000 |
| Mradi wa kupandisha hadhi hospital ya Mnazi Mmoja | 1,125,200,000 | | | 1,125,200,000 | 0 | | 1,125,200,000 |
| Mradi wa Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja | | 10,000,000,000 | | | | | 10,000,000,000 |
| **Jumla ya Fungu(H02)** | | | | | | | **49,772,000,000** |
| **JUMLA YA FUNGU H01 na HO2** | | | | **66,801,151,000** | **84,386,200,000** | **77,964,086,000** | **239,151,436,000** |

**Kiambatisho Namba 7:** Muhtasari wa Makusanyo ya Wizara ya Afya 2023/2024

| Kifungu | KASMA | MAELEZO | Makadirio ya Makusanyo kwa Mwaka 2023/24 |
|---|---|---|---|
| **H0101** | | **Ofisi Kuu Pemba** | |
| | 1422051 | Huduma za Uchunguzi wa Afya | 142,658,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | **142,658,000** |
| **H0103** | 1422015 | Huduma za Maabara | 749,981,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | **749,981,000** |
| **H0104** | | **Programa ya Kinga na Elimu ya Afya (PH0101)** | |
| | 1422035 | Shahada ya Maradhi ya kuambukiza | 596,000,000 |
| | 1422050 | Huduma za Daktari na orodha ya Wafanyakazi na Abiria | 90,000,000 |
| | 1422051 | Huduma za uchunguzi wa Afya | 1,370,000,000 |
| | 1422078 | Ukodishwajiwa wa Maeneo ya Kibiashara | 30,000,000 |
| | 1422124 | Mapato ya UVIKO 19 | 2,000,583,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | **4,086,583,000** |
| **HO105** | | **Program ya Tiba (PH0102)** | |
| | 1422095 | Ada ya Usajili wa Tiba Asili | 132,659,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | **132,659,000** |
| **HO106** | | **Idara ya Uendeshaji na rasilimali watu** | - |
| | **Jumla Ndogo** | | |
| **HO112** | | **Taasisi ya Utafiti wa Afya** | - |
| | 1422094 | Mapato ya Utafiti | 100,000,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | **100,000,000** |
| **HO113** | | **Baraza la Wauguzi** | |
| | 1422118 | Usajili na Leseni Wauguzi | 120,000,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | **120,000,000** |
| **HO114** | | **Baraza la Madaktari** | |
| | 1422118 | Usajili na Leseni Madaktari | 160,000,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | **160,000,000** |
| **H0115** | | **Baraza la Mazingira** | |
| | 1422118 | Usajili na Leseni wataalamu wa Afya ya Mazingira | 50,000,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | **50,000,000** |
| **H0116** | | **Bodi ya Hospitali Binafsi** | |
| | 1422118 | Usajili na Leseni kwa Huduma Hospitali Binafsi | 130,000,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | **130,000,000** |
| **H0117** | | **Baraza la Wataalamu wa Maabara** | |
| | 1422119 | Usajili na Leseni Wataalamu wa Maabara | 80,000,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | **80,000,000** |
| | **JUMLA KUU KWA FUNGU H01** | | **5,751,881,000** |
| | H0201 | **Kitengo cha Uongozi na Utawala Mnazi Mmoja Hospital(PH02)** | |
| | 1422078 | Ukodishaji wa Maeneo Kibiashara | 8,200,000 |
| | 1422094 | Mapato ya Utafiti | 249,985,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | **258,185,000** |
| | **H0202** | **Huduma za Uchunguzi na Matibabu** | |
| | 1422073 | Malipo ya Huduma za Afya kwa wagonjwa wenye BIMA | 790,400,000 |
| | 1423003 | Kitengo cha Huduma za Haraka | 300,000,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | **1,090,400,000** |
| | **JUMLA KUU KWA FUNGU H02** | | **1,348,585,000** |
| | | **JUMLA KUU KWA FUNGU HO1 na H02** | **7,100,466,000** |